

2022

WASIFU WA AFYA YA JAMII YA WAKENYA



MJI WA UJASIRI NA AFYA BORA WA BIRMINGHAM



Birmingham
City Council

Wasifu wa Afya ya Jamii ya Kenya

Dibaji ya Mwandishi

Wasifu wa Afya ya Jamii ya Kenya iliagizwa na Halamashauri ya Jiji la Birmingham kukagua ushahidi kuhusu Jumuiya ya Kenya katika Birmingham na Kitaifa. Ripoti inaunganisha ushahidi kuhusu uzoefu, mahitaji na mtokeo za Jumuiya ya Kenya katika anuwai ya afya na viashiria vya ustawi, ikiwemo elimu, ajira, makazi, afya ya akili, ulemavu, matumizi (mabaya) ya dawa na shughuli za kimwili. Inaonyesha vikwazo vingi vya viwango tofauti na ukosefu wa usawa wanaokabiliwa watu wa Kenya kuhusu afya yao na maisha ya kila siku na kuangaza mapungufu yaliyomo katika msingi wa ushahidi uliopo. Hiyo ripoti inaonyesha kwamba afya ya jamii inahaja ya ufuatiliaji wa kina, utafiti, na ushirikiano na jamii za Kenya katika kiwango cha mtaa na kitaifa.

Wasifu wa Afya ya Jumuiya ya Kenya ni sehemu ya mfululizo mpana zaidi wa muhtasari wa Ushahidi zilizobuniwa na Halmashauri ya Jiji la Birmingham ambayo inazingatia jumuiya maalum za maslahi.

Iliyoandikwa kwa ushirikiano na Marya Arian

Mkurugenzi Mkuu wa Kimataifa katika Hawkmoth Consultancy

Hawkmoth ni kampuni ya ushauri ya kimkakati kwa biashara za kimataifa na Serikali.

Yaliyomo

Muhtasari wa Ushahidi wa Jumuiya	8
Muhtasari Utendaji	9
Methodolojia (Mbinu)	15
1. Utangulizi	18
1.1. Mtazamo wa Jumla wa Jumuiya ya Wakenya	18
1.1.1 Demografia.....	18
1.1.2. Historia na Mifumo za Uhamiaji.....	18
1.1.3. Lugha	20
1.1.4. Chakula.....	21
1.1.5. Utamaduni	21
1.2. Muktadha wa Kimataifa	22
1.2.1. Demografia ya Dunia.....	22
1.3. Muktadha wa Kitaifa	24
1.3.1. Demografia ya Kitaifa	24
1.3.2. Utambulisho wa Taifa	25
1.3.3. Nchi ya Kuzaliwa	26
1.3.4. Dini	27
1.3.4. Wasifu wa Umri.....	28
1.4. Muktadha wa Birmingham	29
1.4.1. Idadi ya Watu	29
1.4.2. Lugha	30
1.4.3. Wasifu wa Umri.....	32
2. Wasifu wa Afya ya Jamii.....	33
2.1 Kupata Mwanzo bora katika Maisha	34
2.1.1. Afya ya mama.....	34
2.1.2. Watoto wasiye Riziki na Vifo vya Watoto Wachanga	38
2.1.3. Chanjo za Utotoni, Umaskini, Fetma, and Utayari wa Shule.....	38
2.1.4 Unene (Fetma) wa Utotoni	38
2.1.5 Chanjo za Utotoni.....	39
Uingereza ina mradi wa chanjo ya watoto kwa wote na viwango vya juu vya chanjo kwa jumla. Mpango wa chanjo kwa watoto kwa sasa inajumuisha 5-kwa-1 chanjo ambayo inalinda dhidi ya dondakoo (diphtheria), pepopunda, pertussis, polio na Mafua ya Haemophilus aina b (DTaP/IPV/Hib) inayotolewa kwa umri wa miezi 2, 3 na 4 (sehemu ya msingi) na nyongeza ya awali ya kuanza shule kati ya umri wa miaka 3 na miezi 3 na umri wa miaka 5 (DTaP/IPV or DTaP/IPV).	39
2.1.6 Umaskini wa watoto	40
2.1.7 Utayari wa shule na kupatikana kwa elimu	40

2.2 Afya ya Akili na Usawa	42
2.2.1 Afya ya Akili	42
2.2.2 Matumizi ya Madawa ya Kulevya.....	43
2.2.3 Uvutaji Sigara	44
2.2.4. Pombe	46
2.3 Maisha ya Afya	47
2.3.1. Unene (Fetma)	47
2.3.2. Mlo	48
2.4. Tendaji katika Kila Umri na Uwezo	50
2.4.1 Shughuli za kimwili	50
2.5. Kufanya Kazi Vizuri na KujifunzaVizuri.....	51
2.5.1 Elimu	51
2.5.2 Shughuli za Kiuchumi	53
2.5.3 Makazi	55
2.5.4 Afya kwa Jumla.....	56
2.5.5 Kuharibika kwa Afya kwa muda mrefu, ugonjwa na ulemavu	56
2.6. Kulinda na Kugundua	57
2.6.1 Uchunguzi	57
2.6.2 Afya ya Kijinsia	60
2.6.3 Kifua Kikuu	61
2.7 Kuzeeka vizuri na Kufa vizuri.....	63
2.7.1 Kisukari.....	64
2.7.2 Maradhi ya moyo na mishipa.....	66
2.7.3 Shinikizo la damu	68
2.7.4 Ugonjwa wa Muda mrefu wa Kuzuia Mapafu-Chronic Obstructive Pulmonary Disease (COPD)	69
2.7.5 Saratani	70
2.7.6 Shida ya Akili (ukichaa).....	71
2.7.7 Mwisho wa maisha	72
2.8 Kuziba Mwanja	73
2.8.1. Umri wa Kuishi	73
2.8.2. Umaskini (Kunyimwa)	74
3. Hitimisho.....	75
4. Kiambatisho.....	76
Kiambatisho 1: Mkakati wa Utafutaji.....	76
Kiambatisho 2: Jedwali la Data Ghafi la Takwimu 1: Mtindo wa Uhamiaji kutoka Kenya hadi England na Wales, 2011	79
Kiambatisho 3: Jedwali la Data Ghafi la Takwimu 2: Maeneo 20 za Juu zenye wakazi waliozaliwa Kenya kote Uingereza, 2011	80
Kiambatisho 4: Jedwali la Data Ghafi la Takwimu 4: Wasifu wa Umri wa wakazi wazaliwa wa Kenya katika England na Wales, 2011	82

Kiambatisho 5: Jedwali la Data Ghafi la Takwimu 5: Mtindo wa Uhamiaji Kutoka Kenya hadi West Midlands,2011.....	86
Kiambatisho 6: Jedwali ya Data Ghafi la Takwimu 6: Wasifu wa Umri ya wakazi wazaliwa wa Kenya katika West Midlands, 2011.....	85
Kiambatisho 7: Jedwali la Data Ghafi la Takwimu 7: Shughuli za wakazi wazaliwa wa Kenya kote Uingereza, kwa jinsia (watu)	87
Kiambatisho 8: Jedwali la Data Ghafi la Takwimu 8: Shughuli ya Kiuchumi kwa jinsia, ilivyorekodiwa katika Sensa ya 2011 ya waliozaliwa Kenya; data kuhusu West Midlands	88
5. Marejeleo.....	89

Tarakimu:

Takwimu 1: Mtindo wa Uhamiaji kutoka Kenya hadi England na Wales, 2011	20
Takwimu 2: Maeneo 20 ya juu yenye wakazi wazaliwa wa Kenya kote Uingereza,2011	24
Takwimu 3: Kusanyiko la wakazi wazaliwa wa Kenya.....	25
Takwimu 4: Wasifu wa umri wa wakazi wazaliwa wa Kenya katika England na Wales,2011	28
Takwimu 5: Mtindo wa Uhamiaji kutoka Kenya hadi West Midlands, 2011.....	30
Takwimu 6: Wasifu wa umri ya wakazi wazaliwa wa Kenya katika West Midlands, 2011.....	32
Takwimu 7: Shughuli za wakazi wazaliwa wa Kenya kote Uingereza, kwa jinsia (watu)	54
Takwimu 8: Shughuli za kiuchumi kwa jinsia, ilivyorekodiwa katika Sensa ya 2011 ya waliyozaliwa Kenya; data ya West Midlands	55

Majedwali:

Jedwali 1: Nchi 10 za juu zenye jumuiya kubwa zaidi za diaspora, Desemba 2015..
..... 22

Jedwali 2: Nchi tano zaa juu za idadi ya watu waliozaliwa Afrika katika England na
Wales: 26

Jedwali 3; Kata 10 za juu huko Birmingham zenye idadi kubwa zaidi ya jamii ya
Wakenya 29

Jedwali 4: Kata 5 za juu zenye idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiswahili katika
Birmingham 31

Jedwali 5: Kiwango cha juu cha uzazi kwa wanawake walio na nchi ya kuzaliwa ya
Kiafrika, wanaoishi katika England na Wales 35

Jedwali 6: Idadi ya wanafunzi kutoka Kenya katika vyuo vikuu vya England, 2020/
2021 52

Muhtasari wa Ushahidi wa Jumuiya

Kama sehemu ya kazi ya Kitengo cha Afya ya Umma ya kuboresha kuelewa kwa jumuiya mbalimbali (anuwai) ya Birmingham, tunatengeneza mfululizo wa muhtasari mfupi wa ushahidi ya kuboresha ufahamu wa jumuiya haya na mahitaji zao.

Haya ni malengo ya pamoja kwa kila muhtasari wa ushahidi ambazo ni:

- Kutambua na kujumlisha afya ya kimwili, afya ya akili, tabia ya maisha, na vidhihirisho pana vya maswala ya afya yanayoadhiri hiyo jumuiya maalum kote kitaifa na maeneo za mitaa.
- Kutambua na kutoa muhtasari wa mapungufu katika maarifa kuhusu afya ya Kimwili, afya ya akili, tabia ya maisha na viashiria pana ya maswala yanahusiana na afya ambayo inaweza kuathiri jumuiya hiyo maalum kwa Kitaifa na maeneo ya mitaa.
- Kulinganisha na Kuwasilisha maelezo haya chini ya maeneo 10 muhimu ya kipaumbele yaliyotambuliwa katika Mikakati wa Afya na Ustawi kuhusu Birmingham 2021
- Kushirikiana na Jumuiya za wenyeji kwa ushahidi uliopatikana na mapungufu yoyote.
- Kukuza matumizi ya haya muhtasari kwa Mamlaka za Mitaa (Serikali ya Mtaa) na kwa matumizi ya mfumo mpana kwa jamii na ustawisho wa huduma.

Muhtasari Utendaji

Wasifu (Umbopande) wa Afya wa Jumuiya ya Wakenya imetambua na kutoa muhtasari wa ushahidi wa kimataifa na ya maeneo ya mitaa kuhusu afya, tabia za maisha na vidhihirisho pana za afya zinazoadhiri jumuiya za Wakenya, kote katika Birmingham na kote Uingereza. Inashughulikia mada ya afya kutoka kwa uzazi hadi kwa uzee na kufa viruri pia; inajumuisha masuala za hatari ya hali ya afya kama vile Kisukari, CVD (cardiovascular disease) yaani Ugonjwa wa moyo na mishipa; mada ya kulinda na kugundua kama vile uchunguzi na chanjo; na mada zingine kama vile maarifa na ufahamu kuhusu masuala ya afya yanayoadhiri Wakenya.

Kumekuwa na ushahidi wa kutokuwa usawa wa afya kati ya makabila machache na makundi za wazungu, na kati ya makundi ya makabila machache katika Uingereza kwa muda fulani. Wasifu huu wa jumuiya inalenga kufungua baadhi ya masuala haya, ikizingatia Jumuiya ya Wakenya ya Birmingham.

Kenya ilikuwa sehemu ya Himaya ya Uingereza katika Africa tangu 1895 na ikapata Uhuru mnamo Desemba 1963, na kuwa Mwanachama wa Jumuiya ya Madola mwaka huo huo. Wakati huo moja, Kenya ikawa jamhuri na Rais wa Kenya akiwa mkuu wa nchi, Kenya ilitoa wanajeshi katika Vita vya Dunia I na Vita vya Dunia II, inakadiriwa kuwa karibu milioni 1.4 ya wanajeshi Wafrika walihudumu katika Vita Vya Dunia vya Pili, ambayo ni pamoja na 289,530 katika King's African Rifles (kutoka Kenya, Tanzania, Uganda, na Malawi).

Mwisho wa 1960 na mapema wa 1970, uhamiaji kutoka Kenya ilikuwa hasa ya Wakenya wa asili ya Asia Kusini waliyolazimishwa kutoka kwa nchi. Walipofika, hii jumuiya ya Wakenya wa asili ya Asia Kusini wengi walitua na kuishi Leicester na kwa kiasi kikubwa inaakisi ramani ya uhamiaji ys watu waliyozaliwa India. Katika

Sensa ya 2011, idadi kubwa ya Wakazi wa Unigereza waliyokuwa Wakenya walijitambua kama Wa Asia (69%), ikilinganishwa na Weusi (16%). Kwa hivyo, wasifu wa Kenya itachunguza data ya kabila ya Wahindi na ya Waafrika Weusi, hususana wakati data za asili ya Wakenya ni haba (adimu).

Kwa Wakenya waliyowasili kabla ya 1981 nchini Uingereza (n=82,736), 47% walikuwa wa Hindu, na wa Sikh walichangia 12.5% na 9.7% walikuwa Waislamu. Kwa jumla, wengi wa Wakenya katika Uingereza ni wa Hindu (37%; 51,211), wanafutwa na Wakristo (25%; 33,797), Waislamu (12%; 16,965), na wa Sikh (10%; 14,212).

Sensa ya 2011 ilirekodi idadi ya watu wakazi 11,099 wazaliwa wa Kenya katika West Midlands na 3,988 katika Birmingham huku jamii ikijikita zaidi katika kata za Hall Green, Springfield, Handsworth Wood and Sparkbrook.

Wasifu wa umri wa Jumuiya ya Wakenya ya West Midlands inaakisi wasifu wa umri kote England na Wales, na 62% kati ya umri ya 45 na 64.

Ushahidi na ufahamu kuhusu ukosefu wa usawa wa afya inayokabili Wakenya katika Birmingham imeshatambuliwa kupitia vyanzo mbalimbali vya maarifa.

Ukosefu wa usawa muhimu wa kiafya na pointi zilizotambuliwa ndani ya Wasifu wa Kenya ni:

- Ukosefu wa maelezo maalum kuhusu jumuiya ya Wakenya. Uboreshaji wa ukusanyaji wa data katika kiwango maalum ya Wakenya inahitajika ili kupata uelewaji wa kweli kuhusu ukosefu wa usawa wa afya wanaokabiliwa jamii ya Wakenya ndani ya Birmingham.

- Kulingana na Ukaguzi wa Kenya wa STEPS wa 2015, ni 6% pekee (wanaume 6.8%, kike 5.2%) ya Wakenya wanaopata kiwango ya chini cha iliyopendekezwa cha resheni tano za matunda na mboga kila siku
- Data inaonyesha kwamba kuna kiwango kubwa cha uvutaji sigara ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika, na 11.6% au milioni 2.5 ya watu wazima Wakenya wanatumia tumbaku (19.1% wanaume na 4.5% wanawake).
- Utafiti uliolenga London ya washiriki ya Wakenya Wa Asia ilipata kwamba washiriki walikosoa mfumo wote wa magonjwa ya akili na wafanyikazi wa magonjwa ya akili.
- Wakenya wana uwezekano kubwa zaidi ya kupata kisukari zaidi kuliko jumuiya ya Wafrika wengine.
- Wazee Wafrika Weusi na wa Caribbean (BACE) wana kiwango cha kuenea wa juu wa kupata ugonjwa wa dementia (shida ya akili) kwa mapema wakilinganishwa na watu wazungu wa Uingereza.

Wasifu wa Jamii ya Kenya

Kimataifa, Kitaifa na Muktadha wa Birmingham

137,493

Watu waliozaliwa Kenya katika England na Wales, kulingana na Sensa ya 2011.

Jamii ya Wakenya katika Uingereza

144,000* 2020
137,492 2011
129,356 2001

*uchunguzi wa kila mwaka wa idadi ya watu

3,988

Watu waliozaliwa Kenya katika Birmingham (0.4%); kuna watu 11,099 wazaliwa wa Kenya kote West Midlands (0.2%)

455,889

Wakenya wanaoishi inji ya Kenya kwa sasa; kuna 190k+ barani Ulaya na Uingereza inachangia takriban 80%

Muktadha wa kimataifa

Kulingana na takwimu za Umoja wa Mataifa, **Uingereza inachangia asilimia 33 ya Wakenya walio nje ya nchi** na karibu 80% ya idadi ya Wakenya barani Ulaya.

Kenya ilikuwa sehemu ya **Himaya ya Uingereza barani Afrika** kati ya 1895 na 1963. Kenya ilipata uhuru kutoka Uingereza mnamo Desemba 1963. Wakati huo moja, Kenya ikawa mwanachama wa Jumuiya ya Madola

Miongoni mwa nchi za kuzaliwa zisio Uingereza zenye idadi kubwa zaidi ya washika pasipoti ya Uingereza, raia waliozaliwa Kenya walikuwa na asilimia kubwa zaidi ya **walio na pasipoti ya Uingereza** na kupata Uraia wa Uingereza (86.9%)

Uhamiaji, Lugha na Imani

Uhamiaji

Wimbi kuu la Uhamiaji kutoka Kenya lilitokea kabla ya 1981 (60%), huku wahamiaji wakuu kutoko nchi hiyo walikuwa **Wahindi Wakenya**. Walipowasili, jamii hiya ya Wakenya ya asili ya Asia ya Kusini walikaa zaidi Leicester na kwa kiasi kubwa inaakisi ramani ya uhamiaji ya watu waliozaliwa India

Lugha

Lugha ya taifa ya Kenya ni **Kiswahili**. Katika England na Wales, **15,059** Watu wanatambua Kiswahili kama lugha yao kuu, **82%** kutoka kwao walikuwa wa asili au Makabila ya Kiafrika

Dini.

Wakenya katika Uingereza ni:

- Hindu (37%)**
- Wakristo (25%)**
- Waislimu (12%)**
- Sikh (10%)**

Ukabila

Idadi kubwa ya wakazi wa Uingereza waliokuwa Wakenya wanajitambua kama

- Wa Asia (69%)**
- Ikilinganishwa na Weusi (16%)**


Usambazaji wa jamii ya Wakenya kote Uingereza

Kulingana na Sensa ya 2011, jamii ya Wakenya imejikita zaidi katika:

- London ya nje-Outer London (54,227; 1.1% hususana Harrow 11,706; 4.9% & Brent 7,382; 2.4%) na
- East Midlands (14,297; 0.3%; hususana katika Leicester 7,118; 2.2%).


Jamii ya Wakenya inajikita katika Kata zifuatayo za Birmingham

Kata ya Birmingham	Nambari ya Wakenya	Uwiano ya Kata (%)
Kata ya Hall Green	416	0.3
Kata ya Springfield	385	0.3
Kata ya Handsworth	302	0.2
Kata ya Sparkbrook	211	0.2
Kata ya Acocks Green	148	0.1














Chanzo: BBC Born Abroad: Kenya. Ramani inaonyesha kama maeneo yenye takriban watu sawa yalikuwa na ukubwa sawa, k.m. London yenye wakazi wengi inachukua nafasi zaidi kuliko nyanda za juu za Scotland zilizo na watu wachache.

Wasifu wa Jamii ya Wakenya

Afya ya Akili na Ustawi		Chakula cha Afya na cha bei Nafuu	Kupata mwanzo bora wa maisha		
<p>Afya ya Akili </p> <p>Utafiti uliolenga London na washirik wa Asia kutoka Kenya ilipata kwamba washiriki walikuwa wanakosoa zote mfumo wa ugonjwa wa akili na wafanyakazi wamagonjwa ya akili. washiriki walihisi kwamba wataalam wa siaktria wanapuuzwa wasiwasi wao kuhusu madhara ya madawa ya akili na walisema madawa ya saiktria yalikuwa na nia ya 'kuzimisha' wagonjwa badala ya kuwatibu.</p>		<p>Kula kwa Afya nzuri </p> <p>Utafiti uliofanyika Marekani iligundua kwamba 82.4% ya washiriki Wakenya walifanya 82.4% Jitihada za makusudi ya kula lishe lenye afya</p>	<p>Fetma ya Utotoni </p> <p>Kutumia data ya kabla ya Wahindi kama wakilisho, asilimia ya watoto wenye uzito kupita kiasi wa umri wa miaka 4 to 5 ilipunguka katika kundi la asili ya Wahindi (kutoka 14.9% hadi 13.8%). Ina kiwango cha chini zaidi kati ya makabila yote na 36.5% ya kundi ya walio kati ya umri wa miaka 10 hadi 11 waliokuwa wazito kupita kiasi.</p>		<p>Wanawake wazaliwa wa Kenya wana moja ya viwango vya chini vya kuzaa kati ya wanawake wa Kiafrika wanaoishi England and Wales.</p>
<p>Pombe </p> <p>Hakuna data kuhusu matumizi ya pombe kwa jamii ya Wakenya; ikitumia data ya vikundi yya asili ya Waafrika Weusi na Wahindi kama wakilisho inaonyesha kwamba kundi zote mbili zina asilimia ndogo ya walazwa hospitalini kwajili ya pombe.</p>		<p>Fetma </p> <p>Utafiti uliochapishwa kutoka Marekani ya Washiriki Wakenya (n=51) ilipata kwamba 56.9% walikuwa 56.9% Wenye uzito mkubwa au na fetma</p>		<p>Kwa waliozaliwa 1,402 kwa wanawake waliozaliwa Kenya ilitoa kiwango jumla cha uzazi cha total fertility rate (TFR) of 1.89</p>	
<p>Matumizi ya Mihadarati</p> <p>Kuna kuenea wa utafunati wa Miraa nchini Kenya (36.8%), na wanaume wengi (54.8%), na matumizi ya juu ya madawa mengine kwa wakati moja pamoja na matumizi ya pombe (78.4%) na uvutaji sigara (64.5%). </p>		<p>Uvutaji</p> <p>Data inaonyesha kwamba kuna uvutaji wa kiwango cha juu ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika, na 11.6% au milioni 2.5 ya watu wazima Wakenya wanatumia tumbako (19.1% wanaume na 4.5% wanawake).</p>		<p>Umaskini Utotoni</p> <p>Kwa kukosekana kwa data maalum ya Kenya, kutizama takwimu kuhusu Wahindi na makabila ya Weusi kama wakilisho inaonyesha kwamba 30% ya watoto wanaoishi katika kaya za weusi walikuwa wanaishi katika familia za kipato ya chini, alama kumi zaidi ya wastani wa kitaifa. Hata hivyo, kaya za Wahindi zilikuwa na uwezekano mdogo zaidi wa kuishi katika kipato cha chini na ukosefu wa uwezo ikilinganishwa na vikundi vya makabila zote (17%; asilimia tatu ya alama chini kuliko wastani wa kitaifa)</p>	
		<p>5-kwa-siku </p> <p>Kulingana na uchunguzi wa Kenya wa STEPS ya 2015, 6% pekee (wanaume 6.8%, wanawake 5.2%) ya Wakenya wanakula kiwango cha chini cha resheni 5 zilizopendekezwa za matunda na mboga kila siku, wakati 23% ya watu wazimu wanaongeza chumwi nyingi kwa chakula mezani na 28% wanatumia kiasi kubwa cha sukari ndani ya vinywaji.</p>		<p>Tendaji katika kila umri & uwezo</p>	
		<p>Shughuli za Kimwili </p> <p>Hakuna data au utafiti uliochapishwa kuhusu viwango vya Shughuli za kimwili za jamii ya Wakenya nchini Uingereza.</p> <p>Hata hivyo, utafiti uliochapishwa kutoka Marekani ya washiriki wa Kenya ilipata kwamba 76.5% ya washiriki Wakenya walifanya juhudi ya maksudi ya kufanya mazoezi na 30.6% walifanya angalau siku 5 za mazoezi ya wastani.</p>		<p>Kuchukua Chanjo </p> <p>Kwa vile wengi wa Wakenya wanajitambua kama wa Asia, inafaa kuzingatia kwamba Wahindi wanachukua chanjo kwa kiasi cha juu zaidi, kwa zaidi ya 90% kwa chanjo zote mbili za msingi, na 75% usambazaji ya chanjo ya mwanzo ya msingi na nyongeza kabla ya kuanza shule katika umri wa miaka at 5</p>	

Wasifu wa Jamii ya Wakenya

Kufanya kazi na kujifunza vizuri	Kulinda na Kugundua t	Kuzeeka Vizuri Kufa Vizuri	
<p>Mafanikio Kitaaluma</p> <p>Kwa Kutumia kategoria za makabila ya Waafrika Weusi na Wahindi kama wasilishi kupata ufahamu kuhusu mafanikio ya elimu kwa jamii ya Wakenya inaonyesha kwamba, wanafunzi weusi Waki Afrika walitimiza Progress 8 alama zaidi ya wastani (0.17), wanafunzi Wahindi walipata kiwango cha alama ya pili ya juu ya Progress 8 (0.71)</p>  	<p>Uchunguzi wa Saratani</p> <p>Hakuna data au maarifa kuhusu uchukuaaji kwa jamii ya Wakenya wa vipimo nchini Uingereza. Hata hivyo, utafiti juu ya uchukuaaji wa vipimo vya Pap smear kati ya wahamiaji Wakenya nchini Uholanzi iligundua kwamba nia ya kushiriki ilizuliwa na vikwazo kama vile:</p> <ul style="list-style-type: none"> • lugha, • Maoni kuhusu mfumo wa matunzo ya afya, • Upendeleo wa GP mwanamke na kutozoea utamaduni geni. 	<p>Kisukari</p> <p>7.8% Utafiti uliyochapishwa kutoka Marekani na washiriki Wakenya (n=51) iligundua kwamba kati ya vikundu sita vya wahamiaji wa makabila ya Kiafrika, Wakenya walikuwa na uwezekano zaidi ya kupata ugonjwa wa kisukaru (7.8%)</p>	<p>Dementia</p> <p>Wazee Weusi Waki Afrika na Wakaribia -Black African and Caribbean elders (BACE) wana kiwango cha juu ya kupata mapema shida ya akili (Dementia) ikilinganishwa na Wazungu wenyeji wa Uingereza</p> 
<p>Bila shughuli za kiuchumi</p> <p>18.9% </p> <p>30.5% </p>	<p>Afya ya Kijinsia</p> <p>Utafiti umepata kwamba jamii wanaoathirika zaidi na janga la UKIMWI/VVU - AIDS/HIV nchini Uingereza ni raia wa Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe, na Congo.</p>	<p>Ugonjwa wa Moyo na Mishipa</p> <p>7.8% Inakadiriwa kwamba vifo kutokana na CVD nchini Kenya ni 13.8%. Vifo vianvyoongoza vya CVD ni Kiharusi (6.1%, wanaume 5.8%, wanawake 6.4%) magonjwa ya moyo ya ischemic (4.6%, wanaume 4.7%, wanawake 4.6%)</p> 	<p>Mwisho wa Maisha</p> <p>Utafiti uliyohusisha washiriki wa Kenya (8%) ilipata katika sampuli ya uchunguzi kwamba watu walio na ugonjwa wa akili pamoja na watunzaji wao kawaida walianza kutafuta msaada kutoka kwa familia ya karibu kisha kufuatilia kwa kushauriana na madaktari wa huduma ya msingi.</p> 
<p>Makazi</p> <p>Wengi ya waliotoka Kenya (78.9%) wanaoishi katika West Midlands anamiliki mali; inaweza kuwa nyumba inayomilikiwa moja kwa moja au ya rehani / mkopo au umiliki wa pamoja.</p> 	<p>Kifua Kikuu (TB)</p> <p>Mnamo 2020, watu waliozaliwa Kenya walichangia (kesi 46) 1.1% za kesi ya TB nchini Uingereza, na muda wa wastani wa miaka 17 years kutoka kuingia hadi kutaarifiwa tangu kuwasili Uingereza.</p>	<p>Ugonjwa wa muda mrefu wa kuzuia mapafu-(COPD)</p> <p>Hakuna takwimu kuhusu kuenea kwa Ugonjwa wa Muda Mrefu wa Kuzuia Mapafu (COPD) kwa jamii ya Wakenya katika Uingereza.</p> <p>Nchini Kenya, magonjwa sugu ya kupumua yanasababisha takriban 1.73% ya vifo (wanaume 1.92%, wanawake 1.5%). Sababu kuu za COPD ni pamoja na:</p> <ul style="list-style-type: none"> • uvutaji tumbako, • uchafuzi wa hewa ya ndani, • uchafuzi wa hewa ya nje na • Vumbi na kemikali za kazini. 	<p>Kuziba mwanya</p> <p>Umaskini</p> <p>Kwa vile 80% ya Wakenya katika West Midlands wanamiliki nyumba zao kwa kikamilifu au wana rehani, na pia wana kiwango ndogo sana ya kutokuwa na ajira, hakuna uwezekano kwamba wakenya nchini Uingereza wanakabiliwa na Umaskini / Kunyimwa.</p> 

Methodolojia (Mbinu)

Utafutaji wa Uchunguzi ulifanyiwa na Timu ya Jumuiya za Afya ya Umma kwa kutumia anuwai ya hifadhidata kama vile National Data Sources, NOMIS (Office for National Statistics), na PubMed kutambua maelezo kuhusu jumiya ya Wakenya kwajili ya Wasifu huu. Maneno muhimu ya utafutaji na vichwa vya mada vinavyohusiana na mada hizo zilitambuliwa. Marejeleo yote yaliyotumika ndani ya wasifu huu zimeainishwa katika maelezo ya mwisho. Kwa utafutaji wa awali wa uchunguzi, njia zifuatazo zilichunguzwa:

a. Vyanzo vya data vya Kitaifa

Data ya NOMIS:

Data imetolewa kwa kikabila (asili) kutoka kwa Sensa ya 2011 inayopatikana katika <https://www.nomisweb.co.uk/>. Ikumbukwe kwamba data ya hivi karibuni sana ya kabila inayopatikana ni kutoka sense ya 2001 na 2011, kwa hivyo hitimisho yoyote inayofikiwa kutokana na utumizi wa data hii na maelezo inapaswa kufanywa kwa tahadhari. Data ya sensa inayofuata inapaswa kutolewa mwisho wa Juni 2022.

Afya ya Taifa ya Umma yaani National Public Health (PHE fingertips) na vyano vya data vya serikali yaani government data sources (ons.gov.uk and gov.uk):

Data imetolewa mahali taarifa husika za ngazi ya jumuiya ya Kenya iliyopatikana.

Ripoti za Sekta ya Kitaifa ya hiari na ya jumuiya:

Hizi zimetambuliwa kupitia Google Scholar na tovuti za kitaifa, hususana mahali data husika za ngazi ya jumuiya ya Wakenya na maelezo yalipatikana, kama vile:

- Kisukari Uingereza – Diabetes UK (<https://www.diabetes.org.uk/>)
- Public Health England (sasa imebadilishwa na kuwa UK Health Security Agency and Office for Health Improvement and Disparities
(<https://www.gov.uk/government/organisations/public-health-england>))

b. Utafutaji wa PubMed

Kuongozea, uchunguzi wa PubMed kupitia <https://pubmed.ncbi.nlm.nih.gov/> ulifanyika. Utafutaji wote ulifanyika kutumia neno muhimu “Kenyan” pamoja na maneno ambayo yalikuwa mahususi na mada ya wazo. Mifano ya haya yamewekwa pamoja katika mkakati wa utafutaji. (Kiambatisho 1).

c. Fasihi ya Kijivu

Mahali vyanzo vya maelezo hazikuwa zimetambuliwa kupitia a au b, utafutaji zaidi kupitia Google, Google Scholar, na PubMed kwa kutumia maneno maalum ya utafutaji wa mada ulifanyika. Makaratasi ambazo zilikuwa maalum kwa Uingereza zilijumuishwa k.v, data na habari inayotokana na ripoti za kiwango za maeneo ama kitaifa na/ au ukaguzi.

Matokeo kutoka kwa mapitio ya kimfumo ya kimataifa na kitaifa na kiwango kikubwa cha elimu ya magonjwa ya mlipuko na utafiti wa ubora yaani qualitative research studies yalizingatiwa ili yajumuishwe. Matokeo ya utafiti ya kimataifa yalijumuishwa ikiwa yanachukuliwa kuwa ya kulinganishwa au husika kwa idadi ya watu wa kitaifa.

Zaidi ya hayo, “snowballing” au “kuongezeka haraka”- mbinu ambapo utafiti wa ziada husika inatambuliwa kutoka kwa orodha ya marejeo husika na nukuu za utafutaji wa awali au Makala iliyochapishwa – pia ilitumika. Makaratasi ziada zilitambuliwa kutoka kwa orodha ya marejeo kwa kutumia mbinu hii, ambapo rasimali hizi nyongeza

ziliimarisha msingi wa maarifa. Kwa jumla, utafutaji zilikomeshwa kwa mwaka wa 2000 kuendelea mbele, hata hivyo mara kwa mara, maelezo ya zamani yalizingatiwa mahali maelezo yaliadimika.

d. Ujumuishaji na Uchambuzi wa Data

Matokeo yaliyopatikana kutoka kwa utafutaji wa awali yalipitiwa upya na Timu ya Jumuiya za Afya ya Umma dhidi ya mkakati wa utafiti (Kiambatisho 1). Makala yaliyotumika katika hati hii ndio zilichambuliwa, kutambuliwa, na kurejelewa kwa kina na mada zingine katika ripoti nzima.

1. Utangulizi

1.1. Mtazamo wa Jumla wa Jumuiya ya Wakenya

1.1.1 Demografia

Kulingana na sensa¹ ya 2011, kuna watu 137,492 wazaliwa wa Kenya katika England na Wales. Mahususi, ilirekodiwa kwamba kuna Wakenya 135,966 katika England, 1,526 katika Wales, 2,743 katika Scotland² na 301 katika Ireland³ ya Kaskazini. Katika Uchunguzi wa Kila Mwaka wa Idadi ya Watu ya 2020-21 ilirekodi kwamba wazaliwa wa Kenya 144,000 ni wakazi wa Uingereza^{4 5}.

Kiwango cha ukuaji cha idadi ya wazaliwa wa Kenyan-born katika Uingereza imepunguka: kutoka 1991 hadi 2001 idadi ya watu waliyozaliwa Kenya iliongezeka kwa 15% (kutoka 112,441 hadi 129,356), ikilinganishwa na kutoka 2001 hadi 2011 wakati idadi ya watu iliongezeka kwa 6.3% pekee (kutoka 129,356 hadi 137,492)⁶. Hata hivyo, inafaa kuzingatia kwamba Sensa hiyo ilirekodi ongezeko kubwa ya idadi ya watu Waafrika Weusi kati ya 2001 na 2011. Mnamo 2001, Sensa ilirekodi Waafrika Weusi 494,669 katika England na Wales, ambayo iliukuwa 0.9 % ya jumla ya watu wote. Idadi hii iliongezeka hadi 989,628 katika Sensa ya 2011, iliyowakilisha 1.8 % ya idadi jumla ya watu, kupanda kwa 100.1 % katika muongo huo⁷. (kipindi cha miaka 10).

1.1.2. Historia na Mifumo za Uhamiaji

Kama inavyoonyeshwa kwenye takwimu 1, wimbi kuu la Uhamiaji kutoka Kenya ilikuwa mbele ya 1981 (60%). Mwishoni wa miaka ya 1960 na mwanzoni wa miaka za 1970, Uhamiaji kutoka Kenya ilikuwa hasa ya kikabila ya Wakenya wa Asia Kusini waliyolazimishwa kutoka kwa nchi. Baada ya kuwasili, wengine wa jumuiya hii ya

Wakenya wa Asia Kusini walikaa Leicester na kwa kiasi kubwa inakisi ramani ya uhamiaji kwa watu waliyozaliwa India⁸.


Kenya inapatikana kwenye pwani ya Afrika Mashariki na inapakana na Tanzania kwa Kusini, Uganda kwa Mashariki na Sudan ya Kusini na Ethiopia katika upande wake wa Kaskazini. Makali ya magharibi ya nchi inapakana na Somalia na Bahari ya Hindi. Pamoja na Somalia na Ethiopia, nchi hizo tatu pamoja zinajulikana kama Pembe ya Afrika. Tangu 1981, kumekuwa na ongezeko kubwa ya wimbi ya uhamiaji kutoka Kenya; uhamiaji wa hivi karibuni kutoka nchi hiyo inahusisha kabila ya Wakenya Waafrika Weusi⁹.

Kenya ilikuwa sehemu ya Himaya ya Uingereza katika Afrika kati ya 1895 na 1963. Kenya ilipata uhuru kutoka kwa Uingereza mnamo Desemba 1963, na ikawa mwanachama wa Jumuiya ya Madola mwaka huo huo. Wakati huo, Kenya ikawa Jamhuri na Rais wa Kenya kama mkuu wa nchi. Kama sehemu ya Himaya ya Uingereza, Kenya ilichangia majeshi wakati wa Vita Vya Kwanza vya Dunia na Vita Vya Pili vya Dunia. Inakadiriwa kuwa karibu milioni 1.4 million ya Wanajeshi Waafrika walihudumu katika Vita vya Pili vya Dunia, iliyojumuisha 289,530 katika King's African Rifles (kutoka Kenya, Tanzania, Uganda, na Malawi)¹⁰.

Moja ya vipengele muhimu katika Uhamiaji kutoka Kenya ni Uhamiaji wa Jumuiya ya Wahindi kutoka Kenya kwenda Uingereza badala ya Waafrika Weusi Wakenya. Kwajili ya Safari hii ya hatua mbili, jumuiya ya Wakenya Wahindi ni kabila tofauti maalum ikilinganishwa na diaspora ya Asia ya Kusini kutoka India, Pakistan na Bangladesh. Wahindi Wakenya wanaitwa "wahamiaji mara mbili" au 'twice migrants', baada ya kukamilisha safari ya hatua mbili, kwanza kutoka bara ndogo la India kwenda kwa chaguo la mataifa ya Afrika Mashariki kisha badaye kwenda Uingereza.

Uhamiaji kutoka Bara ndogo la India kwenda Afrika Mashariki ilianza mwisho wa karne ya kumi na tisa. Ukanda wa Afrika Mashariki iligawanywa kati ya Ujerumani na Uingereza katika miaka za 1890, kutengeneza fursa za kiuchumi na ikashawishi uhamiaji kutoka Asia Kusini. Maeneo ya Afrika Mashariki yalipata uhuru mwanzoni wa miaka za 1960 na serikali zao zikapitisha sera za kiuchumi za Uafrika wakizuia vibali vya kazi na leseni za biashara kwa wasio raia. Hilo ilichochea uhamiaji mkubwa wa Jumuiya ya Wa Asia wa Kusini kutoka Kenya kwenda Uingereza¹¹.

Takwimu 1: Muundo wa Uhamiaji kutoka Kenya hadi England na Wales, 2011



Chanzo: *Sensa ya 2011, Jedwali CT0562*

1.1.3. Lugha

Kenya ni nchi yenye makabila mengi na makabila zaidi ya 40 ikiwa na lahaja na lugha nyingi za kienyeji. Lugha ya Kitaifa ya Kenya ni Kiswahili (jina la asili Kiswahili), na lugha rasmi ni Kiswahili na Kiingereza¹². Katika England na Wales, watu 15,059 walirekodi Kiswahili kama lugha yao kuu, 82% ambao walikuwa wa urithi wa makabila ya Kiafrika¹³.

Katika wazungumzaji wa Kiswahili katika England na Wales, 12,353 wamerekodi asili wao kuwa Mwafrika Mweusi¹⁴. Vilevile, katika wazungumzaji wa Kiswahili walio Weusi Waafrika katika Uingereza, 5,020 walikuwa Wakristo na 6,720 Waislamu¹⁵. Ikizingatiwa kwamba wengi wa Wakenya katika Uingereza ni wa Kikabila ya Wahindi, lugha kuu zinazozungumzwa na jumuiya zitakuwa za Asia ya Kusini. Kulingana na Sensa ya 2011, lugha kumi kuu bora ‘zingine’ katika Uingereza zilikuwa pamoja na Punjabi (watu 273,000), Urdu (269,000), Bengali (221,000) na Gujarati (213,000) iliyoonekana kama la pili, tatu, nne na tano kwa lugha ‘zingine’ zinazozungumzwa zaidi kwa mtiriiko huo¹⁶.

1.1.4. Chakula

Kama nchi ya makabila mbalimbali, vyakula vya Kenya vina ushawishi wa tamaduni nyingi. Chakula ya Kitaifa ya Kenya zinachukuliwa kuwa nyama choma (nyama ya ngombe au mbuzi inayochomwa na kuliwa na ugali – unga wa mahindi, na kachumbari – saladi ya mboga). Vyakula vya pwani wa Kenya vina ushawishi wa Kiarabu na Asia Kusini na ni pamoja na vyakula kama Pilau (wali na nyama kupikwa kwa mchuzi), chapati (mkate was bapa laini), na madafu (maji ya nazi yaliyochukuliwa kutoka kwa matundi mbichi)¹⁷. Hii inalinganishwa na vyakula vya kanda ya kati ya Kenya ambayo inajumuisha vyakula vya nyama vinavyoliwa na wanga kama viazi¹⁸. Huku vyakula vikuu vya jamii ya Waluo na Waluhya wanaopatikana karibu na Ziwa Victoria ni samaki, wakazi wa mijini Kenya wanapenda vyakula mbalimbali kulingana na asili yao¹⁹.

1.1.5. Utamaduni

Watu wengi Mashuhuri nchini Uingereza walizaliwa Kenya, wapakata umaarufu katika sekta kadhaa. Hii ni pamoja na mwanabiolojia mashuhuri na mwandishi,

Richard Dawkins aliyezaliwa Nairobi na kuhamia England akiwa na umri wa miaka nane. Wakenya wengine mashuhuri nchini Uingereza ni pamoja na Mwingereza Mlemavu wa mbio za kiti cha Magurudumu ya Olympiki, Anne Wafula Strike MBE, mwendesha baiskeli Chris Froome OBE, Mwanasiasa wa Uingereza Baron Hain PC, na mwakilishi wa Benchi la Wabunge huru katika Nyumba ya Mabwana (House of Lords), Baroness Prasher CBE PC.

1.2. Mukadha wa Kimataifa

1.2.1. Demografia ya Dunia

Kulingana na takwimu ya Umoja wa Mataifa, Uingereza inahesabu kuwa na 33% ya idadi ya watu Wakenya ng'ambo na karibu 80% idadi ya Wakenya barani Ulaya (tizama takwimu 1). Data ya Umoja wa Mataifa kuhusu 'jumla ya hisa za Wahamiaji' inakadiri kuwa mwaka 2015 zaidi ya watu 455,000 kutoka Kenya walikuwa wanaishi inje ya mipaka za nchi²⁰. Takwimu zifuatazo zinaonyesha jumuiya kumi za juu za ughaibuni za Wakenya.

Jedwali 1: Nchi kumi za juu zinazo jamii kubwa zaidi za Wanadiaspora wa Kenya, Desemba 2015

Nchi	Idadi ya Watu
JUMLA	455,889
1. Ufalme wa Muungano wa Uingereza & Ireland Kaskazini	151,073
2. Marekani (Amerika)	105,467

3.	Uganda	43, 512
4.	Canada	27, 929
5.	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	27, 247
6.	Australia	17, 850
7.	Afrika Kusini	17, 686
8.	Ujerumani	15, 034
9.	Sudan Kusini	9, 558
10.	Italia	3, 641

Chanzo: UN: Divisheni ya Idadi ya Watu – Mwenendo wa hisa za uhamiaji wa Kimataifa; Wahamiaji kwa Wankoenda na Asili, Jedwali 16²¹

Mwaka 2018, Kenya ilipokea takriban £556 milioni, kuifanya kuwa mpokeaji wa 11th kubwa zaidi wa pesa zinazotumwa kutoka Uingereza, sawa na takriban 0.8% la Pato la Taifa ya Kenya yaani GDP²². Kenya na Uingereza wana uhusiano wa muda mrefu na ushirikiano wa karibu katika sekta muhimu za elimu, biashara na uwekezaji. Uingereza ndio mwekezaji mkubwa sana wa kigeni wa Ulaya katika Kenya; baadhi ya Uwekezaji mkubwa wa Uingereza ni katika huduma za kifedha za Kenya, mawasiliano ya simu, kemikali, sekta za ukulima na viwanda. Kwa sasa, kuna karibu ya kampuni za uwekezaji za Uingereza 100 ziliyopo Kenya, zenye zina dhamani ya zaidi ya STG £2.0 billion²³. Vile vile, Uingereza ndiyo nchi ya pili muhimu ya uuzaji wa nje kwa biashara ya Kenya, na biasharanje zikiwemo chai, kahawa na mazao ya bustani.


1.3. Mukstadha wa Kitaifa

1.3.1. Demografia ya Kitaifa

Kama inavyoonyeshwa katika takwimu 2 na 3, hapo chini, idadi kubwa ya Wakenya inapatikana katika Kaskazini Magharibi ya London, hususana katika Harrow na Brent, ikifuatwa na Leicester. Uwepo wa jami katika maeneo haya inaonyesha kwamba kategoria ya wazaliwa wa Kenya ina uwezekano ya kuwasilisha kikundi cha kabili la India kwa vile inaashiria ramani ya Uingereza ya Wakazi wa Uingereza wa India.


Kulingana na Sensa ya 2011, kuna Wazaliwa wa Kenya 3,988 wakazi wa Birmingham, mojawapo ya makazi makubwa ya jumuiya ya Wakenya Waingereza.

Takwimu 2: Maeneo 20 ya juu yenye wakaazi wazaliwa wa Kenyan kote Uingereza, 2011



Chanzo: Sensa ya 2011, Takwimu QS203EW_Nambari

Takwimu 3: Viwango vya Wakazi wazaliwa wa Kenya



Chanzo: Picha ya ramani kutoka BBC²⁴ (Ramani inaonyesha nchi kama maeneo zenye idadi ya watu takriban sawa zilikuwa za saizi moja; London yenye watu wengi inachukuwa nafasi nyingi zaidi kuliko Nyanda za Juu za Uskoti zenye wakazi wachache.)

1.3.2. Utambulisho wa Taifa

Katika Sensa ya 2011, kiasi kubwa cha wakazi wa Uingereza waliokuwa Wakenya walijitambua kama wa Asia (69%), ikilinganishwa na Weusi (16%)²⁵. Kuna habari chache kuhusu ukubwa wa jumuiya mbalimbali katika eneo ya kabila la Waafrika weusi (Black African). Utafiti umegundua kwamba wanobainisha katika kategoria ya “Mweusi yoyote mwengine wa asili ya / Mwaafrika/ Mkaribian ’ kwa kiasi kikubwa inahesabu kwa chini ukubwa kamili ya hizi jamii²⁶.

Utafiti iliyochapishwa²⁷ imegundua kwamba kategoria ya ‘nchi za kuzaliwa’ inatoa tu kipimo elekezi ya saizi ya baadhi ya vikundi vidogo vya makabila tofauti na kwa jumla ni kipimo duni cha wakala kwa asili za kikabila²⁸. Kwa mfano, uwiano ya juu

cha wakazi wazaliwa wa Kenya, Tanzania, and Uganda waliyotambuliwa kuwa wa Asia (69%, 68%, na 58%, mtawalia), ikilinganishwa na Weusi (16%, 17%, na 33%, mtawalia)²⁹³⁰. Kinyume chake, wakazi wa Uingereza 93% ya wazaliwa wa Ghana na 92% ya wazaliwa wa Nigeria walijitambua kama Weusi³¹.

1.3.3. Nchi ya Kuzaliwa

Kati ya nchi zisizo za Uingereza za kuzaliwa uwiano wa juu kabisa ya walio na pasipoti ya Uingereza, raia Wazaliwa wa Kenya walikuwa na asilimia kubwa ya kuwa na pasipoti ya Uingereza na kupata uraia wa Uingereza (86.9%)³². Kuna raia wa Uingereza 125,000 (kinyume na raia wa nchi ya kuzaliwa au mataifa mengine) miongoni mwa raia waliyozaliwa Kenya wanaoishi Uingereza³³. Kwa baadhi ya makabila, nchi ya kuzaliwa ni wakala duni kuhusu ukabila (asili) ya 'Mwafrika Mweusi', kwa mfano katika Sensa ya 2001, 10.5 % ya wazaliwa wa Kenya walijitambua kama 'Mwafrika Mweusi'.³⁴

Kama inavyoonekana kwenye jedwali 2, idadi kubwa sana ya Wafrika waliyozaliwa Uingereza wanatoka nchi zenye mahusiano ya kikoloni; hasa, Afrika Kusini, Nigeria, Zimbabwe, Kenya, Ghana na Somalia³⁵.

Jedwali 2: Nchi tano za Juu za idadi ya watu waliozaliwa Afrika katika England na

Wales:

Nchi	Idadi ya Watu
Nigeria	191,183
Afrika Kusini	191,023
Kenya	137,492

Zimbabwe	118,348
Somalia	101,370

Chanzo: *Sensa ya 2011, Jedwali QS213EW, Nchi ya kuzaliwa*


1.3.4. Dini

Miongoni mwa Wakenya waliyowasili mbele ya 1981 (n=82,736), 47% walikuwa Hindu, wa Sikh walihesabiwa kuwa 12.5% na 9.7% walikuwa Waislamu³⁶. Kwa jumla, wengi wa Wakenya nchini Uingereza ni wa Hindu (37%; 51,211), wakifuatwa na Wakristo (25%; 33,797), Waislamu (12%; 16,965), na wa Sikh (10%; 14,212)³⁷. Tofauti na maumbo wa kidini ya Jumuiya ya Wakenya katika Uingereza, Sensa ya Kenya ya 2019 ilirekodi jumla ya watu 47.2 million na makadirio ya 85.5% ya idadi jumla ya watu kuwa Wakristo, 11% Waislamu (wengi wao wakiwa wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi jirani ya Somalia³⁸), chini ya 2% ni wa Hindu, Sikh, Baha'i, na wale wanaofuata imani mbalimbali za kimapokeo³⁹. Waprotestanti wasio wainjilisti wanahesabiwa kuwa 33% ya idadi ya watu, Wakatoliki wa Roma 21%, na madhehebu mengine ya Kikristo, wakiwemo waprotestanti wa Kiinjili, Taasisi ya Makanisa ya Afrika na Makanisa ya Imani halisi yaani kiorthodoksi, 32%⁴⁰.

1.3.4. Wasifu wa Umri

Kikundi cha wazaliwa wa Kenya katika Uingereza ina wasifu wa umri mkubwa, ikilinganishwa na vikundi vya makabila mengi madogo mengine. Wasifu wa Umri wa Jamii ya Kenya inaakisi uhamiaji wa mapema wa kikundi hiyo, na 60% walihamia kwenda England na Wales kabla ya 1981. Kizazi cha pili na cha tatu cha wakazi wa Kenya wanaweza kurekodi Uingereza kama nchi yao ya kuzaliwa, Mwingereza kama utambulisho wao wa kitaifa na Mu Asia au Muhindi kama kabila au asili,

Takwimu 4: Wasifu wa Umri ya wakazi wazaliwa wa Kenya katika England na Wales, 2011



inayomaanisha kwamba kuzaliwa kwa vizazi vya baadaye havijaakisiwa katika Wasifu wa umri ya Wakenya.

Chanzo: Sensa ya 2011, Jedwali CT0561

1.4. Mukadha wa Birmingham

1.4.1. Idadi ya Watu

Sensa ya 2011 ilirekodi wakazi wazaliwa wa Kenya 11,099⁴¹ katika West Midlands na 3,988 katika Birmingham⁴², huku jamii ikijikita zaidi katika kata za Hall Green, Springfield, Handsworth Wood na Sparkbrook (takwimu 3).

Hiyo Sensa ya 2001 ilirekodi wakazi wazaliwa wa Kenya 3,769 (0.4% ya jumla ya wakazi wa jiji)⁴³; hiyo iliongezeka hadi 3,988 (uwiano sawa: 0.4% ya jumla ya wakazi wa jiji) katika mwaka 2011⁴⁴. Kama inavyoonyesha kwenye takwimu hapa chini, inayoakisi mifumo ya uhamiaji kutoka Kenya hadi Uingereza, wimbi kuu la uhamiaji kutoka Kenya hadi West Midlands ilifanyika kabla ya 1981 na takriban 70% waliwasili katika kipindi hiki cha muda. Tangu 1981, hakujakuwa na wimbi mkubwa la uhamiaji kutoka Kenya kwenda Midlands Magharibi (West Midlands).


Takwimu 3: Kata 10 zaa juu za Birmingham zinazo idadi kubwa zaidi ya jamii ya Wakenya

Kata ya Birmingham	Nambari ya Wakenya	Uwiano ya kata (%)
Kata ya Hall Green	416	0.3
Kata ya Springfield	385	0.3
Kata ya Handsworth Wood	302	0.2
Kata ya Sparkbrook	211	0.2
Kata ya Acocks Green	148	0.1
Kata ya Aston	187	0.1

Kata ya Billesley	153	0.1
Kata ya Bordesley Green	106	0.1
Kata ya Brandwood	76	0.1
Kata ya Edgbaston	137	0.1

Chanzo: Sensa ya 2011; Halmashauri ya Birmingham (Birmingham City Council)⁴⁵

Takwimu 5: Mtindo wa Uhamiaji kutoka Kenya hadi West Midlands, 2011



Chanzo: Sensa ya 2011 CT0562

1.4.2. Lugha

Kulingana na Sensa ya 2011, kuna wazungumzaji wa Kiswahili 1,250 katika West Midlands, na watu 364⁴⁶ katika Birmingham waliyotoa Kiswahili kama lugha yao kuu; ni 2.4% pekee ndiyo wazungumzaji wa Kiswahili katika Uingereza wanaoishi Birmingham na wengi wao wakiishi katika mtaa au wilaya ya Ladywood (131)⁴⁷. Kata tatu za juu zenye nambari kubwa ya wasemaji Kiswahili katika Birmingham ni Aston, Nechells, Lozells na East Handsworth.

Jedwali 4: Kata 5 za juu za idadi kubwa ya wazungumzaji Kiswahili katika Birmingham


Kata ya Birmingham	Nambari ya Wasemaji wa Kiswahili
1. Aston	44
2. Nechells	37
3. Lozells na East Handsworth	35
4. Ladywood	26
5. Soho	24

Chanzo: *Sensa ya 2011, Halmashauri ya Birmingham (Birmingham City Council), QS204*

1.4.3. Wasifu wa Umri

Jumuiya ya Wakenya katika West Midlands ina wasifu wa umri mkubwa kwa 62% wakiwa kati ya umri ya 45 na 64, na inaakisi wasifu wa umri wa jamii hiyo kote England na Wales. Watu wa umri ya 45 hadi 64 wanachangia 62% of ya jamii ya

Takwimu 6: Wasifu wa Umri ya wazaliwa wa Kenya wakaazi wa West Midlands, 2011



Wakenya katika West Midlands (6,914), wakati wa umri ya 0 hadi 19 yachangia 5% tu (552).

Chanzo: *Sensa ya 2011, Jedwali CT0561*⁴⁸

2. Wasifu wa Afya ya Jamii

Tofauti kubwa za kiafya zipo kati ya makabila madogo na watu Weupe, mfumo unaoakisiwa katika jamii ya Wakenya. Sehemu zifuatazo zinawasilisha na kuonyesha takwimu muhimu za afya na data kutoka kwa mkusanyiko wa vyanzo. Kila sehemu inaangazia matokeo muhimu na umbizo la nukta ya vitone, kabla ya kuwasilisha taarifa za kina zenye ushaidi. Matokeo yote ni muhimu katika kufahamisha sera, ambayo inaweza kutumika kushugilikia masuala za afya ya Wakenya ndani ya Uingereza na hususana Birmingham.

2.1 Kupata Mwanzo bora katika Maisha

Matokeo Muhimu

- Wanawake wazaliwa wa Kenya wana kiwango cha kuzaa cha chini zaidi miongoni mwa wanawake wa Kiafrika wakazi wa England na Wales.
- Wengi wa Wakenya wanajitambulisha kama wa Asia, Wahindi wana kiwango cha juu zaidi ya uchukuaji wa chanjo za utotoni, kwa **zaidi ya 90%** kwa chanjo zote mbili msingi, na **75%** uchukuaji wa chanjo la msingi na nyongeza ya kabla kuanza shule inayotolewa katika umri wa miaka 5
- Kutumia data la kundi la kabila la wahindi kama wakilisho, asilimia ya watoto walio na uzito kupita kiasi wa umri ya 4 hadi 5 ilipunguka katika kundi la kabila ya wahindi (**kutoka 14.9% hadi 13.8%**).
- Kulingana na Sensa ya 2011, watoto waliyozaliwa **1,402** kwa wanawake wazaliwa wa Kenya ilitowa kiwango cha uzazi cha **1.89**, kiwango cha kuzaa cha chini kuliko wamama wa Kisomali (**4.19**) na Nigeria (**3.32**), lakini juu kuliko kiwango cha wamama wa Zimbabwe (**1.83**) na wa Afrika Kusini (**1.79**).

2.1.1. Afya ya mama

Kuna data na maelezo madogo kuhusu afya ya mama ya akina mama wa Kenya katika Uingereza. Wanawake waliozaliwa Kenya wana moja ya kima cha uzazi ya chini sana miongoni mwa wanawake wa Kiafrika wanaoishi katika England na Wales. Kulingana na Sensa ya 2011, waliozaliwa 1,402 kwa wanawake waliozaliwa Kenya ilitoa kiwango cha jumla cha uzazi cha 1.89, kima cha uzazi cha chini kuliko cha wamama kutoka Somalia (4.19) na Nigeria (3.32) lakini kima cha juu kuliko kina mama wa Zimbabwe (1.83) wa South Afrika Kusini (1.79). Kwa upana zaidi, afya ya mama na maradhi kwa wanawake Weusi hutajwa mara nyingi katika utafiti uliyochapishwa; Utafiti wa hivi karibuni uligundua kwamba Wanawake Weusi wako kitakwimu na uwezekano wa kufa mara nne zaidi wakati wa kujifungua kuliko wanawake Weupe katika Uingereza⁴⁹.

Kiwango cha jumla cha uzazi yaani total fertility rate (TFR) inafafanuliwa kama nambari ya wastani ya watoto ambayo kikundi cha wanawake wanaweza kuzaa katika maisha yao yote ya kuzaa. TFR inatoa ufahamu katika kiwango cha uzazi katika mwaka fulani na si lazima kuwakilisha idadi ya wastani ya watoto yenye kikundi cha wanawake wataokuwa nao katika maisha yao.⁵⁰ Utafiti⁵¹ imegundua kwamba TFR ni ya juu kati ya Wanawake Weusi wa Kiafrika katika Uingereza, ikilinganishwa na vikundi vya makabila mengine madogo. Mwaka 2014, kuzaa kwa akina mama waliyozaliwa Africa ilichangia 5% ya wazaliwa hai⁵². Kulingana na Sensa ya 2011, kati ya wanawake wanaoishi England na Wales lakini wamezaliwa Afrika walikuwa na TFR ya 2.76 –hii ilikuwa TFR ya juu zaidi kati ya Wanawake wanaoishi England na Wales lakini wamezaliwa katika eneo lolote la dunia⁵³.

Data kuhusu kiwango cha uzazi inaonyesha, kwa jumla kwamba jumuiya kubwa za wahamiaji katika Uingereza kinatoa kiwango cha juu zaidi cha uzazi. Kwa mfano, kuzaliwa kwa watoto 5,654 na wanawake waliyozaliwa Somalia ilitoa TFR ya 4.19, ya pili kwa ukubwa katika Afrika Kusini mwa Sahara. Kwa kinyume chake, kuzaliwa kwa watoto 1,402 kati ya wanawake waliozaliwa Kenya ilitoa kiwango cha uzazi wa jumla ya 1.89, kima cha chini cha uzazi kuliko akina mama kutoka Somalia na Nigeria (3.32) lakini kiwango cha juu kuliko cha akina mama wa Zimbabwe (1.83) na wa Afrika Kusini (1.79) katika Uingereza.

Jedwali 5: Kiwango cha Jumla cha Uzazi cha wanawake walio na nchi ya Kuzaliwa ya Afrika, wanoishi katika England na Wales

Nchi ya Kuzaliwa ya Mama	Total Fertility Rate (TFR) (Kiwango cha jumla cha uzazi)	Nambari ya waliyozaliwa ya 2011 (England na Wales)
--------------------------	---	--

Somalia	4.19	5,654
Nigeria	3.32	7,476
Uganda	2.52	916
Kenya	1.89	1,402
Zimbabwe	1.83	2,837
South Africa	1.79	4,430

Chanzo: *Sensa ya 2011 na Aspinall (na wengine) et al.*⁵⁴

MBRRACE-UK imetoa ufahamu juu ya viwango vya magonjwa ya uzazi na utofauti wa rangi zilizopo katika huduma ya afya ya uzazi. Hiyo ripoti ya MBRRACE-UK *'Enquiries into Maternal deaths and morbidity' 2020* 'yaani *'Uchunguzi juu ya vifo vya uzazi na magonjwa' 2020* inatoa ufahamu muhimu. Ilhali haina takwimu haswa za kina mama kutoka Kenya, ripoti ilifichua kwamba Wanawake Weusi kwa kitakwimu wana uwezekano kubwa wa kufa wakati wa kujifungua kuliko wanawake Weupe katika Uingereza^{55 56}. Inaangazia tofauti kadhaa katika takwimu za matokeo ya uzazi, pamoja na asili (kabila),ografia na nafasi ya kijamii na kiuchumi. Imepata ripoti za Wanawake Weusi kupuuzwa ama kuambiwa kwamba wana kuza au kutia chumvi wakilalamika kuhusu maumivu⁵⁷. Vile vile, mada zingine zinazojitokeza kutoka kwa ripoti ya *Lessons learned to inform maternity care from the UK and Ireland Confidential Enquiries into Maternal Deaths and Morbidity 2017-19 report*⁵⁸ yaani (*Uelewa wa kini ilifanyika ili kufahamisha huduma ya uzazi kutoka Uingereza na Ireland, Uchunguzi wa Siri juu ya vifo vya uzazi na magonjwa 2017-19*) pamoja na kutojihisi salama, kupuuzwa au kufukuzwa, kunyimwa vituliza maumivu kutokana na ubaguzi wa rangi, na uchokozi ndogo uliyoenea kusababisha madhara au dhiki⁵⁹.

Kwa vile kuna asili mia kubwa ya raia wa Kenya wa urithi wa Kihindi, maelezo kutoka kwa akina mama wazaliwa wa India inaweza kusaidia kubaini hatari waliopitia akina mama wa Kenya. Kume kuwa na mwelekeo chanya kwa kuzingatia hatari zinazoweza kama za vifo vya uzazi kwa wamama waliozaliwa India. Kutoka 2016 hadi 2018 akina mama wazaliwa wa India walikuwa mara 2.16 katika hatari ikilinganishwa na wanawake waliozaliwa Uingereza, na takwimu hii ikionyesha kupunguka hadi mara 0.86 ya hatari kutoka 2017 hadi 2019.

Ripoti ya Uzazi ya MBRRACE UK iligundua wakati wa kufanya uchambuzi wa viwango vya vifo vya uzazi kulingana na nchi ya kuzaliwa ya mama, kutoka 2017 hadi 2019 kwamba kulikuwa na 7.42 kwa 100,000 vifo vya uzazi katika Uingereza miongoni mwa akina mama waliozaliwa India, ikilinganishwa na vifo 8.66 kwa 100,000 ya wanawake wazaliwa wa Uingereza.

Ripoti ya *2011 Confidential Enquiries into Maternal Deaths in the UK*⁶⁰-(Uchunguzi wa Kisiri kuhusu Vifo vya Uzazi katika Uingereza) ilitambua wahamiaji wajawazito ambao wanaweza kuwa hawafahamu lugha ya Kiingereza au utamaduni kuwa na uwezekano wa kuathirika. Iligundua kwamba chini ya robo ya wanawake waliofariki mnamo 2017-19 (23%) ambao mahali zao za kuzaliwa yalijulikana kuwa kuzaliwa inje ya Uingereza; 22% ya hao wanawake walijulikana sio raia wa Uingereza, na Uraia haukurekodiwa kwa wengine zaidi ya 20%⁶¹. Kwa jumla, 6% ya wanawake waliofarika hawakuwa raia wa Uingereza, ingawa hiyo inaweza kuwa makadirio ya chini kwa vile uraia haikurekodiwa kwa wanawake 7%.⁶² Ufahamu huu ni muhimu hasa kwa wanawake wahamiaji wa hivi karibuni kutoka Kenya.

2.1.2. Watoto wasiye Riziki na Vifo vya Watoto Wachanga

Kuna maelezo chache kuhusu watoto wasie riziki na vifo vya watoto wachanga katika jamii ya Wakenya. Hata hivyo, kwa vile idadi kubwa ya Wakenya wanajitambua kama wa Asia (69%), ikilinganishwa na Weusi (16%), na kwa jumla karibu 60% ya Wakenya katika Uingereza ni wa Hindu, Waislamu, na Sikh, hii sehemu inatumia uwakilisho kama data kutoka kote kwa Wafrika Weusi na vikundi vya Wahindi kutoa ufahamu kuhusu masuala ya watoto wasio riziki na vifo vya watoto wachanga ndani ya jumuiya ya Wakenya.

Utafiti uliyochapishwa umegundua kwamba, kutoka 2014 hadi 2019, tofauti kubwa kurekebishwa⁶³ katika watoto wasio riziki yalikuwa ya juu zaidi kwa watoto wa vikundi vya Asili ya Weusi Wafrika (3.83) ni chini sana kati ya Wahindi (1.71)⁶⁴. Idadi kubwa ya watoto wa asili ya Waafrika Weusi (39%) walikuwa katika maeneo ya umaskini sana, ambayo ilikuwa inahusishwa na hatari nyongeza ya watoto wasio riziki 1.50 kwa 1000 ya wazaliwa. Idadi ya watoto wasio riziki yaliyofanyika bila sababu kujulikana ilikuwa juu zaidi kwa watoto wa asili ya kihindi (52%).

2.1.3. Chanjo za Utotoni, Umaskini, Fetma, and Utayari wa Shule

Hakuna data au maarifa kutoka kwa utafiti uliyochapishwa inayohusisha uchukuaji wa chanjo za utotoni, umaskini wa watoto na (fetma) unene kwenye diaspora ya Kenya katika Uingereza, wala data kuhusu mafikio ya elimu ya wanafunzi wa Kenya. Ili kutoa ufahamu katika mada hizo, sehemu hii inatumia data kutoka kwa vikundi vya Waafrika Weusi na Wahindi kama wakilishi.

2.1.4 Unene (Fetma) wa Utotoni

Kwa vile hauna data inayolenga Kenya, takwimu kuhusu kundi cha Wafrika Weusi ikitumika kama wakilisho inaonyesha kwamba kati ya watoto wa umri wa 4 hadi 5 na

umri wa 10 hadi 11, Watoto Weusi wa Kiafrika walikuwa na uwezekano mkubwa wa kuwa wanene kupindukiwa (fetma) katika 2017/18. Karibu theluthi moja (30.8%) yao katika kundi la umri ya 4 hadi 5 walikuwa wanene kupindukiwa, na 46%⁶⁵ ya walio na umri wa 10 hadi 11 walikuwa fetma, idadi kubwa zaidi kati ya makundi za kabila zote.

Kwa kulinganisha, asili mia ya watoto wanene katika umri wa 4 hadi 5 ilipungua katika kundi la kabila ya Wahindi (kutoka 14.9% hadi 13.8%)⁶⁶. Karibu 13.8% ya wao katika kundi la umri wa 4 hadi 5 walikuwa wanene, idadi ya chini zaidi katika kundi zote za makabila na 36.5% ya walio katika kundi la umri wa 10 hadi 11 walikuwa wanene⁶⁷. Kutokana na Wakenya wengi kujitambulisha kama wa asili ya Asia, inawezekana kwamba data kuhusu kabila la India inakamata idada ya watoto wa Kenya walio wanene au fetma.

2.1.5 Chanjo za Utotoni

Uingereza ina mradi wa chanjo ya watoto kwa wote na viwango vya juu vya chanjo kwa jumla⁶⁸. Mpango wa chanjo kwa watoto kwa sasa inajumuisha 5-kwa-1 chanjo ambayo inalinda dhidi ya dondakoo (diphtheria), pepopunda, pertussis, polio na Mafua ya Haemophilus aina b (DTaP/IPV/Hib) inayotolewa kwa umri wa miezi 2, 3 na 4 (sehemu ya msingi) na nyongeza ya awali ya kuanza shule kati ya umri wa miiaka 3 na miezi 3 na umri wa miaka 5 (DTaP/IPV or DTaP/IPV)⁶⁹.

Hakuna data maalum kuhusu uchukuaji wa chanjo kwa jamii ya Wakenya, hata hivyo, data kuhusu uchukuaji wa chanjo katika London kwa jamii ya Kiafrika na ya Wahindi inaweza kutoa ufahamu. Kwa ukumbusho, London ina kiwango cha chini ya uchukuaji wa chanjo ikilinganishwa na kusambazwa kwa chanjo kwa Uingereza nzima. Hii inawezekana kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu wa makabila tofauti, sawa na Birmingham ambayo ni mji wa makabila mengi sana (uchukuaji wa chanjo kwa chanjo za msingi za DTaP/IPV/Hib/HepB ni 87.7% katika London, sawa

na West Midlands ambapo uchukuaji wa dosi la chanjo ni 87.9%⁷⁰). Kama wakilishi, uchukuaji wa chanjo za Utotoni kwa Waafrika⁷¹ katika London kati ya 2006/7 na 2010/11 inaonyesha kiwango cha juu cha 90% na zaidi ya 90% kwa chanjo mbili za msingi, mtawalia. Hata hivyo, uchukuaji unapungua kufika karibu 65% kwa nyongeza ya chanjo kabla ya shule kuanza inayotolewa kwa umri wa miaka 5⁷².

Kwa vile wengi ya Wakenya wanajitambua kama wa Asia, ni muhimu kuzingatia kwamba Wahindi wana uchukuaji wa kiwango kubwa zaidi, kwa zaidi ya 90% kwa chanjo zote mbili ya msingi, na 75% ya uchukuaji wa chanjo kwa chanjo ya mwanzo ya msingi na chanjo ya nyongesa kabla ya kuanza shule inayotolewa kwa umri wa miaka 5⁷³.

2.1.6 Umaskini wa watoto

Kwa ukosefu wa data maalum ya Kenya, kuangalia takwimu kuhusu Makabila ya Weusi kama wakilishi inaonyesha kwamba 30% ya watoto wanaoishi katika kaya au nyumba za Weusi waliishi katika familia zenye kipato cha chini, pointi asili mia kumi juu kuliko wastani wa kitaifa⁷⁴. Kaya za Wahindi, ambazo zinaakisi asili mia kubwa ya jumla ya nyumba au kaya za Wakenya, walikuwa na uwezekano mdogo sana wa kuishi katika mapato ya chini na kunyimwa uwezo wakilinganishwa na vikundi vya makabila zote (17%; pointi asilimia 3 chini kuliko wastani wa kitaifa)⁷⁵.

2.1.7 Utayari wa shule na kupatikana kwa elimu

Kwa kutumia kategoria za Waafrika Weusi na wa Kabila za Kihindi kama wakilishi kupata ufahamu kuhusu Jamii ya Wakenya kuhusu kupatikana kwa elimu inonyesha, kwamba wanafunzi Waafrika Weusi walitimiza alama ya Progress 8 ya juu zaidi kuliko wastani (0.17). Data wakilishi kuhusu wanafunzi Wahindi inaweza kutumika kujenga picha ya watoto wa Kenya, kwajili ya asilimia kubwa ya Wakenya kuwa wa

asili ya India. Wanafunzi wa Kihindi walifikisha kiwango cha pili cha juu ya alama ya Progress 8 (0.71) – ndiyo kikundi cha kabila yenye uwezekano wa chini kupitia mapato ya chini pekee, na mapato ya chini na kunyimwa uwezo zote pamoja. Kuna uwezekano kwamba kupatikana kwa elimu kwa wanafunzi wa Kenya inatokezea katika kategoria zote mbili.

2.2 Afya ya Akili na Usawa

Matokea Muhimu

- Utafiti kuhusu mitazamo ya matumizi ya mirungi/miraa miongoni mwa Wakenya nchini Kenya inaonyesha matumizi ya madawa nyingi kati ya watafunaji wa miraa, hasa pombe (**78.4%**) na uvutaji wa sigara (**64.5%**).
- Kuenea kwa uvutaji sigara nchini Kenya ni ya juu ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika, na **11.6% au milioni 2.5** ya Watu wazima Wakenya wanatumia tumbaku (**19.1%** wanaume na **4.5%** wanawake).
- Kiwango cha uvutaji sigara kwa Wakenya ni chini kuliko cha Uingereza; **13.8%** mwaka 2020. Inawezekana kuwa jamii ya Wakenya katika Uingereza ina kiwango cha chini cha uvutaji kuliko wenzao Wazungu.
- Utafiti uliolenga London ya washiriki Wakenya wa Asia iligundua kwamba washiriki walishtumu mfumo wa matibabu ya mgonjwa ya akili na wafanyikazi wa maradhi ya akili.
- Wanaume Waafrika Weusi na Wahindi wana kiwango cha chini cha kulazwa hospitalini kutokana na matatizo maalum ya pombe kuliko wanaume Wazungu Wakingereza (0.5% na 2% dhidi ya 79%)

2.2.1 Afya ya Akili

Utafiti uliolenga London⁷⁶ na washirika wakiwemo Wa-Asia Wakenya, Waafrika Weusi, wa Caribbean Weusi, Wahindi, na watu Wakisomali (n=103) iliripoti kwamba washiriki walikosoa zote mifumo ya saikatria na wafanyikazi wa saikatria. Washiriki walihisi kwamba wataalamu wa saikatria walipuuza wasiwasi wao kuhusu madhara ya madawa ya kutibu magonjwa ya saikatria na vilevile kwamba madawa ya akili yalilengo 'kuzimua' wagonjwa badala ya kuwatibu⁷⁷.

Utafiti⁷⁸ juu ya athari ya uhamiaji na maswala ya afya ya akili kati ya Wakenya katika Amerika pia ilitoa kiasi cha ufahamu muhimu. Washiriki wa Kenya katika utafiti huo waliripoti ubaguzi, utenganishaji, aibu⁷⁹, kutoa fidia ya juu⁸⁰, mkazo wa kitamaduni⁸¹, ubaguzi, hisia ya unyonyaji⁸², vikwazo vya lugha, migogoro za familia kati ya vizazi tofauti, na vikwazo vya kijamii na kiuchumi, yote ambayo yaliweka Wahamiaji katika hatari kubwa ya kupata matatizo ya afya ya akili⁸³. Inaendelea kudai kwamba mchanganyiko wa kuishi na matatizo ya afya ya akili, kujaribu kuzoea mazingara mapya na mawasiliano machache ya kijamii yanaowasaidia, na rasilmali chache za kiuchumi inaweza kuzuia maendeleo na kujihusisha na huduma⁸⁴. Wahamiaji wa Kenya walielezea kwamba mchakato wa ujumuishaji kama ya “changamoto”, pamoja na kupoteza utambulisho wa kitamaduni na uhamisho na mshiriki mmoja akieleza kwamba “Nilikatishwa tamaa, Nilipata dhiki na kwa machache, nilifikiria kurudi nyumbani, nilifikiria kununua tikiti na kupanda ndege ya kunirudisha nyumbani”⁸⁵. Ikiangalia kwa upeke wazee wahamiaji wa umri kubwa, utafiti uligundua matumizi ya hali ya chini ya huduma rasmi za afya ya akili wakilinganishwa na wote katika idadi ya wahamiaji kwa jumla na wazee wasio wahamiaji, na lugha ikiwa kikwazo⁸⁶.

2.2.2 Matumizi ya Madawa ya Kulevya

Hakuna habari kuhusu jamii ya Wakenya na utumizi wa madawa ya kulevya katika Uingereza. Hata hivyo, utafiti juu ya mitazamo kuhusu matumizi ya miraa/ mirungi miongoni ya Wakenya inapatikana.

Utafiti⁸⁷ imegundua kuenea kwa kutafuna kwa miraa/mirungi katika Kenya kuwa 36.8% (n= 306), wengi kuwa wanaume (54.8%). Baadhi ya washiriki katika utafiti waliripoti angalau dalili moja ya kisaikolojia (16.8%), na kuenea kwa juu kwa vipindi hivi miongoni mwa wanawake (19.5%)⁸⁸. Inaangazia vilevile matumizi ya juu ya

mchanganyiko wa madawa ya kulevya kwa wakati moja miongoni mwa watafunaji wa miraa/ mirungi, hususana matumizi ya pombe (78.4%) na uvutaji wa sigara (64.5%)⁸⁹. Kwa vile takwimu hizi ni za shughuli nchini Kenya, sio thabiti kudhani kwamba picha inafanana na ya watu wa jamii ya Kenya katika Uingereza. Ikitumia data ya jamii ya Waafrika Weusi katika Uingereza kama wakilisho, Uchunguzi wa Uhalifu wa Uingereza yaani the British Crime Survey (BCS) iliunganisha seti ya data ya miaka tatu (2006-09), inayoonyesha kiwango cha matumizi ya mihadarati kati ya watu wazima kutoka kwa asili ya Mweusi au Mweusi Mwingereza yalikuwa ya chini kuliko kwa Weupe au Vikundi vya Wachanganyiko⁹⁰. Wale kutoka kwa asili ya Weusi wa Karibea (Caribbean) walikuwa na matumizi ya kiwango ya juu ya bhangi na mihadarati yoyote (7.9% na 8.7% mtawalia) kuliko asili ya Mweusi Mwafrika (2.7% na 3.5% mtawalia)⁹¹.

2.2.3 Uvutaji Sigara

Hamna data au habari kuhusu kiwango cha uvutaji sigara katika jamii ya Wakenya nchini Uingereza. Hata hivyo, ASH⁹² imegundua kwamba wakati watu wanahamia kuja Uingereza wengi wanakuja kutoka kwa nchi zenye mfumo tofauti wa kisheria wa udhibiti wa tumbaku, mtazamo tofauti wa kitamaduni juu ya matumizi ya tumbaku na uwezekano wa kiwango cha juu cha uvutaji wa sigara.

Data⁹³ inaonyesha kwamba kiwango cha kuenea kwa uvutaji sigara nchini Kenya ni ya juu ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika, na 11.6% au milioni 2.5 ya watu wazima wa Kenya wanatumia tumbaku (19.1% wanaume na 4.5% kike). Ingawa hii ni ya chini kuliko ya Uingereza; mwaka 2020, 13.8% ya watu wa umri wa miaka 18 na zaidi walivuta sigara⁹⁴. Inawezekana basi kwamba jamii ya Wakenya katika Uingereza ina kiwango cha chini cha uvutaji sigari kuliko kundi la asili ya Weupe.

Hitimisho linaungwa mkono zaidi na utafiti uliyochapishwa kutoka Marekani. Uchunguzi ulijumuisha jamii sita za Wahamiaji wa Kiafrika, pamoja na washiriki wa Kenya (n=51) na ikagundua kwamba 96.1% wa washiriki wa Wakenya hajawai kuvuta sigara⁹⁵. Kwa muktadha wa kitamaduni ya jamii ya Wakenya, Kenya ni mtengenezaji mkuu wa tumbaku na ina uhusiano mkubwa na tasnia ya tumbaku na uvutaji sigara ya kiwango ya juu⁹⁶. Data kutoka Chuo cha Bath ambayo inategemea takwimu kutoka kwa Wizara ya Afya ya Kenya inaonyesha kwamba 11.6% ya idadi ya watu wazima (milioni 2.5 ya watu wazima, wengi wao wakiwa wanaume) wanatumia bidhaa za tumbaku, na 10% wa vijana miaka 13-15 (karibu 13% ya wavulana 7% ya wasichana)⁹⁷. Miongoni ya watu wazima wa miaka 18-69, 13% wanatumia tumbaku na kiwango ya juu kuwa kwa wanaume (23%) kuliko wanawake (4%). Mwaka 2007, Bunge ya Kenya ilipitisha Sheria ya Udhibiti wa Tumbaku ya 2007 (Tobacco Control Act 2007) (TCA), kuidilisha Mkataba wa Mfumo wa Udhibiti wa Tumbaku (the Framework Convention on Tobacco Control) (FCTC)⁹⁸.

Ikitumia data ya Uingereza⁹⁹ ya kundi la asili ya Weusi, takwimu kutoka 2017 inaonyesha wanaume na wanawake Weusi wana kiwango cha chini cha uvutaji sigara ikilinganishwa na wenzao Wazungu (15% na 7%, kulinganishwa na 22% na 14%, mtawalia). Matokeo haya yanaakisi data ya ONS inayoonyesha kwamba kiwango cha uvutaji ni cha chini katika vikundi vya makabila madogo kuliko katika kikundi cha Weupe¹⁰⁰. Vile vile, utumizi wa data ya waliozaliwa India kama wakilishi ili kuelewa kuenea kwa uvutaji sigara miongoni mwa Jamii ya Wakenya, inaonyesha kwamba wakazi wazaliwa wa India wana kiwango cha chini zaidi cha 'wavutaji wa sasa' (4.3%) pamoja na kiwango cha juu zaidi cha wale 'hawajawai kuvuta sigara' (87.5%)¹⁰¹.

2.2.4. Pombe

Matumizi dhulma ya pombe ni moja ya sababu kuu ya kuchangia vifo vya mapema na ulemvu na ina athari kubwa kwa afya ya umma¹⁰². Matumizi mabaya ya pombe yanakadiriwa kugharimu Huduma ya Afya ya Taifa yaani NHS takriban bilioni £3.5 kila mwaka na jumuiya kwa jumla bilioni £21 kila mwaka.¹⁰³

Ingawa hakuna data au habari kuhusu matumizi ya pombe kwa Jamii ya Wakenya katika Uingereza, utumizi wa data ya vikundi vya asili ya Wahindi na Waafrika Weusi kama wakilishi inaonyesha kwamba vikundi zote mbili zina asilimia ndogo ya kulazwa hospitalini kuhusiana na pombe. Matumizi dhulma ya pombe ni moja ya sababu kubwa inyochangia vifo vya mapema na ulemavu na ina athari ya kiwango kubwa kwa afya ya umma¹⁰⁴. Matumizi mabaya ya pombe yanakadiriwa kugharimu Huduma ya Afya ya Taifa yaani NHS karibu bilioni £3.5 kila mwaka na kwa jumuiya kwa jumla bilioni £21 kila mwaka.¹⁰⁵

Kulingana na data ya 2014/15 ya England, wanaume Wafrika Weusi na and Wahindi wanachangia 0.5% na 2% ya wanaolazwa hospitali kwajili ya matatizo maalum za pombe, kufuatana, zote mbili ziko chini kuuliko ya Waingereza Weupe (79%)¹⁰⁶. Vile vile, wanawake wote Wafrika Weusi na Wahindi wanachangia 0.4% ya wanaolazwa hospitalini kwajili ya matatizo maalum ya pombe katika England, kwa kiasi kikubwa chini kuliko Wanawake Weupe (84.5%)¹⁰⁷. Kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa kwamba matumizi ya pombe na kulazwa hospitalini kuhusiana na pombe ndani ya jamii ya Wakenya ni ndogo katika Uingereza.

2.3 Maisha ya Afya

Matokeo Muhimu

- Utafiti kutoka Marekani ya washiriki Wakenya with Kenyan (n=51) iligundua kwamba **56.9%** walikuwa wazito kupita kiasi au fetma.
- Hakuna data au Utafiti uliyochapishwa kuhusu lishe ya jamii ya Wakenya nchini Uingereza. Utafiti kutoka Marekani ya washiriki Wakenya (n=51) iligundua kwamba **82.4%** ya washiriki walifanya jitihada za maksudi kula lishe ya afya njema.
- Kulingana na uchunguzi wa Kenya wa STEPS ya 2015, **6% pekee** (wanaume 6.8%, wanawake 5.2%) ya Wakenya wanapata resheni tano zinazopendekezwa za matunda na mboga kila siku, wakati **23%** ya watu wazima wanaongeza chumvi kwa chakula mezani.

2.3.1. Unene (Fetma)

Hamna data au habari ya Jamii ya Wakenya katika Uingereza inayozingatia kuenea kwa tatizo la kunona sana. Hata hivyo, utafiti uliyochapishwa kutoka Marekani ya Washirika Wakenya (n=51) iligundua kwamba 56.9% walikuwa wanene sana au kuwa fetma¹⁰⁸. Kwa vikundi sita vya Wahamiaji Wafrika, hiyo ilikuwa zaidi ya Wasomali (49.5%) na Wasudan (27.4%), lakini chini kuliko wa Liberia (74.1%) na wa Wahabeshi (Ethiopians) (59.9%)¹⁰⁹. Unene sana na uzito mkubwa zinahusishwa na kuongezeka kwa kiwango cha magonjwa sugu na ni sababu kuu za maradhi yasiyo ya kuambukiza kama magonjwa ya moyo na mishipa, kisukari, na aina fulani za saratani.

Ingawa hamna data na habari kuhusu kiwango cha Unene katika jamii ya Wakenya katika Uingereza, utafiti kutoka 2018 iligundua nchini Kenya kwamba kuenea kwa uzito mkuba na kunenepa kwa wanawake ni cha kiasi cha juu na inaweza kuendelea kuongezeka¹¹⁰. Kuenea kwa uzito kupita kiasi ilikuwa 20.5%, na kuenea kwa fetma

ilikuwa 9.1%, ikionyesha kiwango kikubwa cha wanawake wa Kenya kuwa wanene au na fetma¹¹¹. Iligundua vile vile kwamba wanawake katika maeneo ya mijini wa hali ya juu ya kijamii na kiuchumi wanawakilisha kiasi kikubwa zaidi ya walio wazito au na fetma¹¹². Kwa jumla, nchini Kenya, kuenea kwa uzito mkubwa na fetma ilikuwa juu zaidi kati ya wanawake kuliko wanaume (kwa kiwango cha 17.5% kwa wanaume na 38.5% kwa wanawake kuwa wanene zaidi, na 4.7% kwa wanaume na 13.7% kwa wanawake wakiwa na fetma, mtawalia)¹¹³.

Kutumia data kutoka kwa Health Survey England 2004 ya Wafrika Weusi kama wakilishi kuelewa kuene kwa uzito mkubwa katika Jamii ya Wakenya Uingereza inaonyehsa kiwango kubwa ya Uzito kupindukiwa kwa Wafrika Weusi, pamoja na fetma (BMI zaidi ya 25 kg/m²), ilikuwa 61.8% kati ya wanaume (61.8 %). Kuenea kwa unene, pamoja na fetma, ilikuwa ya juu kuliko idadi jumla ya watu, katika wanawake Wafrika Weusi (69.8%), kiasi ya juu sana katika vikundi vyote. Mduara jumla wa kiuno ilikuwa 90.6cm kwa Wanaume Weusi Wafrika (chini kuliko idadi jumla ya watu: 96.5cm) na 90.2 cm kwa wanawake Weusi Wafrika (juu kuliko idadi jumla ya watu 86.4cm).

2.3.2. Mlo

Hamna data au habari kuhusu mlo ya Jamii ya Wakenya katika Uingereza. Hata hivyo utafiti uliyochapishwa Marekani ikishirikisha Wakenya (n=51) iligundua kwamba 82.4% ya washiriki walifanya jitihada za makusudi kula lishe yenye afya¹¹⁴. Hii ilikuwa zaidi ya vikundi mengi nyingine za wahamiaji wa Kiafrika, pamoja na Wasomali (77.6%), Wahabesha (80.1%) na Wasudan (55.4%). Utafiti pia uligundwa kwamba washiriki waliyokuwa wazee na kuripoti kuelewa Kiingereza vizuri walikuwa na uwezekano kuwa ya kufanya jitihada za makusudi ya kula lishe yenye afya. Kwa

hivyo inafaa kuzingatia kwamba 96.1% ya washiriki wa Kenya waliripoti kuelewa kiingereza vizuri¹¹⁵.

Lishe ya afya ina kazi muhimu ya kuzuia maradhi yasio ya kuambukiza. Ingawa hamna utafiti uliyochapishwa kuhusu mlo ya Jamii ya Wakenya katika Uingereza, kutumia data ya vikundi vya makabila ya asili ya Wahindi na Wafrika Weusi kama wakilishi inaweza kutoa ufahamu muhimu. Kulingana na HSE 2004, miongozo zilizoopendekezwa za kula matunda na mboga tano au zaidi kwa siku yalitimizwa na 23% ya wanaume na 27% ya wanawake katika idadi jumla ya watu. 31% ya wanaume Weusi Waki Afrika walitimiza mapendekezo ya tano kwa siku, na 32% ya wanawake Weusi Waki Afrika walitimiza mapendekezo. Zaidi ya theluthi moja ya wanaume wa Kihindi na wanawake walitimiza mapendekezo ya tano kwa siku (37% na 36%, mtawalia).

Data kutoka Kenya pia inatoa maarifa muhimu. Kulingana na uchunguzi wa STEPS¹¹⁶ wa Kenya wa 2015, ni 6% tu (wanaume 6.8%, wanawake 5.2%) ya Wakenya wanaopata kiwango cha chini cha resheni tano za matunda na mboga zinazopendekezwa kila siku, wakati 23% ya watu wazima wanaongeza chumvi nyingi kwa chakula mezani na 28% wanatumia kiasi kubwa cha sukari katika vinywaji¹¹⁷. Hiyo uchunguzi pia iligundua ufamiaji ya hali ya juu miongoni mwa Wakenya kuhusu hatari kubwa ya kiafya inahusishwa na ulaji wa chumvi nyingi na sukari (87.7% na 91.3% mtawalia), hata hivyo ni takriban nusu ya waliohojiwa walizingatia upunguzo wa hayo kama muhimu sana¹¹⁸.

2.4. Tendaji katika Kila Umri na Uwezo

Matokeo Muhimu

- . Hakuna data au utafiti uliochapishwa kuhusu viwango vya shughuli za kimwili za jamii ya Wakenya nchini Uingereza.
- Utafiti kutoka Marekani ya washiriki Wakenya (inaripoti 76.5% ya washiriki Wakenya walifanya jitihada za maksudi kufanya mazoezi na 30.6% walifanya angalau siku 5 za mazoezi ya wastani.

2.4.1 Shughuli za kimwili

Hakuna data au utafiti uliyochapishwa juu ya viwango vya shughuli kwa jumuiya ya Wakenya katika Uingereza. Hata hivyo, utafii uliyochapishwa kutoka Marekani na washiriki Wakenya (n=51) inatoa maarifa muhimu: 76.5% ya washiriki Wakenya walifanya jitihada za makusudi kufanya mazoezi na 30.6% walifanya angalau siku 5 za mazoezi za wastani¹¹⁹. Hii ilikuwa zaidi ya washiriki Wasomali (50.3% na 26.7%, mtawalia) na Wa Ethiopia (Mahabeshi) (51% na 24.7%, mtawalia)¹²⁰. Utafiti uligundua kuwa watu waliyoripoti kuelewa Kiingereza vizuri walikuwa na uwezekano wa mara 3 zaidi wa kufanya jitihada za maksudi za kufanya mazoezi¹²¹. Washiriki wenye hawakuwa kamwe au mara chache kuwa na shida ya kushughulikia gharama walikuwa na uwezekano mdogo wa kuripoti kufanya jitihada za maksudi ya kufanya mazoezi¹²².

Uchunguzi wa Kenya wa STEPS wa 2015¹²³ iligundua kwamba 6.5% ya watu wazima hawajihusishi na kiwango kilichopendekezwa cha shughuli za mwili. Matokeo haya yote yanadokeza kwamba Wakenya kwa kitamaduni ni wazoefu wa mazoezi ya kimwili, hasa wakilinganishwa na makabila mengine.

2.5. Kufanya Kazi Vizuri na Kujifunza Vizuri

Matokeo Muhimu

- Mnamo 2020/21 kulikuwa na wanafunzi **2,640** kutoka Kenya katika Uingereza, waliochangia 6% ya wanafunzi kutoka Afrika.
- Vyuho vitatu vya juu kwa wanafunzi wa Kenya zilikuwa Chuo cha Coventry, Chuo cha Kent na Chuo cha Brunel.
- Wengi wa wakazi wazaliwa wa Kenya katika Uingereza wako na ajira za taaluma.
- Katika West Midlands, **48%** ya wanaume wazaliwa wa Kenya wana ajira ya wakati wote, ikilinganishwa na **34.1% ya** wanawake wazaliwa wa Kenya.
- **21.7%** ya wanawake wazaliwa wa Kenya katika West Midlands wana kazi za muda, ikilinganishwa na **7%** ya wanaume.
- Vilevile, **18.9%** ya wanaume wazaliwa wa Kenya na **30.5%** ya wanawake hawana shughuli za kiuchumi, na **5.9%** ya wanaume na **4.4%** ya wanawake hawana ajira.
- Wengi ya Wakenya (**78.9%**) wanaoishi West Midlands wanamiliki nyumba zao.
- **71.8%** ya wakazi wa West Midlands kutoka Kenya walihisi wana afya nzuri sana ama wana afya njema, kiwango ya chini kidogo kuliko **76.6%** katika England and Wales. **8.8%** walihisi kwamba wana afya mbaya au siha mbovu sana, zaidi ya wanaoishi kote England na Wales (**6.7%**).
- **76%** ya waliotoka Kenya wanaoishi na matatizo ya afya ya muda mrefu au ulemavu katika West Midlands walihisi kwamba hali hiyo haikuathiri shughuli zao za kila siku, ikilinganishwa na **23.5%** waliohisi kwamba hali inaathiri.

2.5.1 Elimu

Mwaka 2020/21 kulikuwa na wanafunzi 2,640 kutoka Kenya, ambao ni 6% ya wanafunzi wote kutoka Afrika. Vyo vikuu vitatu vy juu vilivyo na idadi kubwa zaidi ya wanafunzi wa Kenya zilikuwa Chuo cha Coventry, the Chuo cha Kent na Chuo cha Brunel (jedwali 6).

Uchunguzi wa Wanafunzi wa Kenya (n=300) wanaotafuta elimu ya juu nchini Uingereza iligundua kwamba wengi wa wanafunzi walipata masomo chanya na maisha chuoni chanya, ingawa baadhi walielezea kuhusu sehemu hasi pia. Hizo zilikuwa pamoja na kuondoka Uingereza bila shahada (tuzo) yoyote, kutokuwa na uwezo wakukamiliza kozi na kutoweza kuzoea Uingereza¹²⁴. Iligundua kwamba waliohojiwa walichagua Uingereza kama mahali pa kusoma ili kupata sifa zinazotambuliwa ulimwenguni, kupata elimu ya juu na kupata ujuzi unaofungua matarajio bora ya ajira katika soko la ajira lenye ushindani¹²⁵.

Wengi ya waliyohojiwa walipata matatizo ya kifedha kwa vile hawakuweza kupata ajira licha ya kuruhusiwa kufanya kazi kwa masaa ishirini. Wengine walipata matatizo kusimamia gharama zisizotarajiwa kama mabadiliko ya kupanda na kushuka ya fedha za kigeni, tozo zisizotarajiwa kulipishwa na vyuo, gharama ya kuvunja mikataba na gharama za maisha¹²⁶. Changamoto nyingine zilikuwa pamoja na mswala za utendaji kama chakula, usafiri, uhamiaji na kusawazisha kazi na masomo, yote haya yaliathiri maendeleo yao ya masomo na matokeo¹²⁷.

Katika utafiti mwingine, mwanafunzi wa Kenya alisema maendeleo ya juu yanawezekana wakati wa kuishi Uingereza lakini alisisitiza umuhimu wa kupata jukumu la kitaaluma badala ya kazi ya kibarua¹²⁸.

Jedwali 6: Idadi ya wanafunzi kutoka Kenya katika vyuo vya England, 2020/ 2021

Eneo / Sehemu ya Utoaji wa Elimu ya Juu	Nambari ya Wanafunzi
JUMLA	2,235

Kaskazini Mashariki	75
Kaskazini Magharibi	210
Yorkshire na The Humber	200
East Midlands	295
West Midlands	280
Mashariki ya England	160
London	460
Kusini Mashariki	385
Kusini Magharibi	170
Open University in England	5


Chanzo: HESA¹²⁹

2.5.2 Shughuli za Kiuchumi

Wengi wa wazaliwa wa Kenya wakazi wa Uingereza wako katika ajira za taaluma, na wanaume wengi na wanawake wa Kenya wanatumika katika ajira za taaluma (takwimu 5). Katika West Midlands, 48% ya wanaume wazaliwa wa Kenya wapo kwenye ajira ya kudumu, ikilinganishwa na 34.1% ya wanawake wazaliwa wa Kenya. 21.7% ya wanawake wazaliwa wa Kenya kwenye West Midlands wapo katika kazi ya muda, ikilinganishwa na 7% ya wanaume. Pia, 18.9% ya wanaume wazaliwa wa Kenya na 30.5% ya wanawake hawana shughuli za kiuchumi, na 5.9% ya wanaume na 4.4% ya wanawake hawana ajira¹³⁰ (jedwali 6).

Kuna idadi kubwa ya wakenya katika sekta ya afya, na wimbi kuu la wauguzi wapya wa Kenya waliosajiliwa ilitendeka kutoka 2001-hadi 2004 (jedwali 7). Kulingana na NHS Digital, hadi Machi 2021, Wakenya 894 walikuwa wanafanya kazi na NHS¹³¹. Kwa miaka mengi serikali za Uingereza na Kenya wamefanya kazi kwa pamoja ili kujenga ushirikiano wa afya. Mwezi Julai 2021, serikali ya Uingereza ilitangaza¹³² kwamba wauguzi wasio na ajira na wafanyikazi wa afya kutoka Kenya watapa nafasi ya kufanya kazi nchini Uingereza kama sehemu ya mpango mpya uliyoombwa na serikali ya Kenya¹³³. Hata hivyo, mpango huo ulisitishwa kutokana na uhaba wa wafanyikazi wa afya na huduma za jamii nchini Kenya¹³⁴.

Jedwali 7: Ajira za wakazi wazaliwa wa Kenya katika Uingereza, kwa jinsia (watu)




Chanzo: *Sensa ya 2011, Takwimu CT0255*

Kama inavyoonyeshwa kwenye Takwimu 8 hapo chini, kuna idadi kubwa zaidi ya wanawake wazaliwa wa Kenya katika West Midlands ambao hawana shughuli za kiuchumi (1,470) kuliko wanaume wazaliwa wa Kenya (908). Kuna wanaume wengi zaidi wazaliwa wa Kenya katika ajira za kudumu kuliko wanawake, wakati wanawake wana uwezekano mkubwa wa kuajiriwa kwa muda. Viwango vya wanafunzi ni sawa

katika jinsia, ilhali kuna zaidi ya mara tatu ya idadi ya wanaume waliojajiri kwa muda wote, kama wanawake.

Jedwali 8: Shughuli za Kiuchumi kwa jinsia, kama ilivyorekodiwa katika Sensa ya 2011 kwa waliozaliwa Kenya; data kutoka West Midlands



Chanzo: Sensa ya 2011 CT0566

2.5.3 Makazi

Kulingana na Sensa ya 2011¹³⁵, wengi ya waliotoka Kenya (78.9%) ambao ni wakazi wa West Midlands ni wamiliki wa nyumba, ama nyumba inamilikiwa moja kwa moja au kwa rehani / mkopo au umiliki wa pamoja (36.9% ya wakazi kutoka Kenya wamemiliki nyumba zao moja kwa moja na 42% wanamiliki nyumba zao kwa rehani/ mkopo au umiliki wa pamoja¹³⁶). Hiyo inaweza kulinginishwa na England na Wales mahali 33.5% ya wakazi kutoka Kenya wanamiliki nyumba zao moja kwa moja na 41.9% wanamiliki nyumba zao kwa rehani/ mkopo au umiliki wa pamoja.

Kulingana na Sensa ya 2011, kaya za Kenya hazina changamoto za msongamano wa watu. Karibu 55.8% za kaya za Kenya zina “hadi watu 0.5 kwa kila chumba”, 40.3% “zaidi ya watu 0.5 na hadi 1.0 kwa kila chumba”, na 0.8% pekee wana “zaidi

ya watu 1.5 persons kwa kila chumba". Hii inaweza kulinganishwa na kaya za Kisomali ambapo takwimu zilikuwa 28.9%, 42.9% and 10.6%, mtawalia¹³⁷.

2.5.4 Afya kwa Jumla

Kwa swala ya afya kwa jumla, 71.8% ya wakazi kutoka Kenya waliyochunguzwa katika West Midlands walihisi wana afya nzuri sana au afya njema, chini kidogo kuliko 76.6% katika England na Wales. Katika West Midlands, 8.8% waliona kwamba wana afya mbaya, au afya mbaya sana zaidi ya wanaoishi kote kwa England na Wales (6.7%)¹³⁸. Kwa waliotoka Kenya katika West Midlands, 13.1% ya walio na umri wa miaka 55 - 64-walihisi kwamba wana afya mbaya au afya mbaya sana wakilinganishwa na 10.1% kote kwa England na Wales katika kundi hilo la umri.

2.5.5 Kuharibika kwa Afya kwa muda mrefu, ugonjwa na ulemavu

Kulingana na uchunguzi wa Tatizo la kKafya wa Muda mrefu au Ulemavu, 76% ya waliotoka Kenya wanaoishi na tatizo la afya la muda mrefu au ulemavu katika West Midlands waliona kuwa haikuathiri shughuli zao za kila siku, ikilinganishwa na 23.5% waliohisi kwamba iliathiri¹³⁹. Kwa tofauti kidogo, katika England na Wales, 80% ya waliotoka Kenya wanaoishi na tatizo la afya la muda mrefu au ulemavu waliona kwamba haikuathiri shughuli zao za kila siku, juu kuliko wa West Midlands; 20% waliohisi iliathiri shughuli zao za kila siku, chini kuliko wa West Midlands. Matokeo katika **sehemu 2.5.4.** na **2.5.5** yanaonyesha kwamba jamii ya Wakenya katika West Midlands kwa jumla walijionyesha kujisikia wagonjwa zaidi kuliko wenzao kote katika England na Wales. Itakuwa muhimu kufanya utafiti wa kina na wa maarifa kuchunguza sababu ya matokeo haya.

2.6. Kulinda na Kugundua

Kulinda na Kugundua Matokeo Muhimu:

- Hakuna data au maarifa kuhusu uchukuaji wa vipimo vya uchunguzi katika jamii ya Wakenya nchini Uingereza. Uchukuaji wa vipimo vya Pap smear kwa wahamiaji Wakenya Kenya nchini Uholanzi iligundua kwamba nia ya kushiriki ilizuiliwa na vizuizu vilivyoonekana kama vile lugha, maoni kuhusu mfumo wa afya, kupendelea kuwa na GP mwanamke na matatizo ya kuzoea mila geni.
- Uchunguzi wa Kenya wa STEPS ya 2015 iliripoti kiwango cha chini cha uchunguzi wa saratani ya mlango wa uzazi mingoni mwa wanawake wa kati wa umri wa 25-49 kwa 14.2%
- Utafiti umegundua kwamba katika jamii za Uingereza zilizo adhirika zaidi na janga la UKIMWI/ VVU walikuwa raia wa Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe, na Congo.
- Mwaka 2020, watu waliozaliwa Kenya walichangia 1.1% za kesi za Kifua Kikuu (TB) nchini Uingereza (46 cases)
- Utafiti uliochapishwa kuhusu uchukuzi wa uchunguzi wa saratani ya maziwa/matiti miongoni mwa vikundi vya wanawake wa makabila tofauti katika London iligundua kwamba 61% ya wanawake Wahindi walihudhuria miadi ya kwanza, na 74% wakahudhuria miadi ya kawaida ya baadaye, ikilinganishwa na 49% ya wanawake Weusi Wafrika waliyohudhuria miadi ya kwanza na 64% wakahudhuria miadi ya kawaida ya baadaye.

2.6.1 Uchunguzi

Hakuna data au habari kuhusu jamii ya Wakenya kuchukua hatua katika uchunguzi nchini Uingereza. Hata hivyo, utafiti¹⁴⁰ juu ya uchukuaji wa vipimo vya Pap smear miongoni ya Wakenya nchini Uholanzi uligundua kwamba nia ya kushiriki ulizuiliwa na vikwazo vinavyoonekana kama lugha, maoni kuhusu mfumo wa huduma ya afya, upendeleo wa daktari wa kike na kutafuta kozoea utamaduni wa nchi geni.

Saratani ya Mlango wa kizazi inayosababishwa na HPV (Human Papillomavirus) ni moja ya saratani zinazoweza kudhibitiwa na kutibiwa, mradi inangunduliwa mapema. Kipimo cha Pap smear ni utaratibu nzuri sana ya kugundua saratani ya mlango wa uzazi. Uchukuaji wa Pap smear miongoni wa jamii za wahamiaji iko chini sana. Utafiti umetambua vikwazo kama lugha, maoni kuhusu mfumo wa huduma ya afya, mapendeleo yakupata daktari wa kike na tatizo la kuzoea utamaduni geni¹⁴¹. Hata hivyo, ukweli ni kwamba utafiti wa STEPS wa 2015¹⁴² (iliyofanyika Kenya) iliripoti viwango vha chini sana vya vipimo vya saratani ya mlango wa uzazi kati ya wanawake wa umri kati ya 25-49 kwa 14.2% ilionyesha kwamba, badala ya vikwazo vya lugha au upendeleo wa madaktari wa kike, kikwazo miongoni ya wanawake wa Kenya, inawezekana kuwa uvamizi na asili ya uchunguzi wa ndani wa kipimo. Utafiti wa Denmark ulidokeza mapendekezo matatu: barua za mualiko kutolewa kwa lugha nyingi isipokuwa lugha ya Kiholanzi; kuanzishwa kwa wiki ya uhamasishaji kuhusu saratani ya mlango wa kizazi; na, programu zilizoimarishwa za uhamasishaji kuhusu uchunguzi na chanjo za lazima na vipimo vya pap kwa wahamiaji wanya waliowasili¹⁴³.

Kutumiwa kwa utafiti uliyofanyika Uingereza¹⁴⁴ kuhusu kundi la Wafrika Weusi kama wakilisho ili kuelewa uchukuaji wa Uchunguzi katika jamii ya Wakenya inaonyesha wanaume Weusi wa Kiafrika wana uwezekano mara mbili hadi tatu ya kugunduliwa na saratani ya tezi kibofu ikilinganishwa na wanaume Weupe, na baadhi wanonekana kuwa na ujuzi mdogo juu ya ugonjwa huo. Utafiti umegundua ukosefu wa maarifa na kuelewa kwa saratani kati ya sampuli ya uchunguzi, ambao mara nyingine walipatiwa taarifa potofu ndani ya jamii ya watu Weusi, ikiwa ni pamoja na dawa za mitishamba. Baadhi ya washiriki waliamini kwamba maumbili zao za kimbari/ kiasili zilikuwa kizuizi jinsi maarifa machache yalitolewa kwao na wataalamu wa afya. Utafiti ulihitimisha haja ya kuongeza ufahamu juu ya saratani ya kibofu tezi katika jamii ya Weusi na

kuelimisha wanaume kuhusu ugonjwa huo na athari zake. Kuongezea, habari zenye msingi wa Ushahidi zinahitajika kutoa elimu kwa wanaume Weusi na kupunguza athari za upotoshaji kuhusu ugonjwa huo na tiba za mitishamba kwa ustawi wao.

Kuongezea, kwa vile wengi wa wa Kenya wanajitambua kiasili kama wa Asia, ingekuwa muhimu kuelewa uchukuaji wa uchunguzi (screening) kati ya jamii ya Wahindi. Utafiti uliyochapishwa¹⁴⁵ kuhusu kuhudhuru kwa uchunguzi wa saratani ya maziwa/ matiti miongoni mwa wanawake kutoka makabila mbali mbali katika London iligundua kwamba 61% ya wanawake Wahindi walihudhuria wito wao wa kwanza, na 74% walifika kwa miadi ya kawaida ya baadaye, ikilinganishwa na 49% ya wanawake Weusi Wafrika na 64% wakihudhuria miadi ya kawaida yanayofuata. Takwimu hizi zinaweza kukamata uchukuaji wa miadi ya vipimo vwa maziwa/matiti ndani ya jamii ya Wakenya.

Inakadiriwa kuwa matukio ya saratani yataongezeka kwa 62.7% hadi takriban kesi 77,894 kila mwaka kufikia mwaka 2030 katika ukuaji wa sasa wa watu. Uchunguzi wa STEPS ya Kenya wa 2015 iliripoti viwango vya chini vya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi miongoni mwa wanawake wa kati ya umri wa 25-49 kwa 14.2%¹⁴⁶. Utambuzi wa mapema inahakikisha matokeo mazuri na ubashiri wa saratani nyingi. Karibu 70% za kesi zinazoripotiwa nchini Kenya hugunduliwa wakati ugonjwa umefika hali mbaya zaidi na wakati kidogo kinaweza kutimizwa, na matokeo ni duni sana¹⁴⁷. Itaweza saidia kufanya utafiti na kutathmini uchukuaji wa vipimo vya saratani kati ya jamii ya Waingereza wa Kenya ili kuelewa vizuri zaidi juu ya vikwazo vinazoweza patikana kuhusu uchunguzi na upimaji.

2.6.2 Afya ya Kijinsia

Hakuna data kuhusu Afya ya kijinsia ya kundi la asili ya Kenya nchini Uingereza. Hata hivyo, utafiti umegunda kwamba jamii katika Uingereza waliothirika zaidi na janga kubwa la Ukimwi/ Virusi vya Ukimwi (AIDS/HIV) walikuwa raia wa Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe, na Congo¹⁴⁸. Nchini Kenya, kuna unyanyapaa fulani kwa wanawake wanoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU), ambao wameathiriwa kupita kiasi na janga hili. Wakati wanawake wanatazamwa kuhitaji mume mmoja, inakubaliwa kitamaduni kwa wanaume kuwa na wake wengi.¹⁴⁹

Kuchunguza Kenya ili kuelewa magonjwa ya zinaa (STIs) katika diaspora ya Uingereza inaonyesha kwamba maambukizi vya VVU yalipunguka kutoka 7.1 % mnamo 2007 hadi 5.6 % mwaka 2012, ingawa maambukizi mapya yanabakia kuwa juu, kwa karibu 100,000 kila mwaka. Kuenea kwa VVU kati ya kundi la 15 hadi 24 ilikuwa 2.1 % mwaka wa 2012, kupunguka kutoka 3.8 % mwaka 2007. Ndani ya kundi hili la umri, wasichana wako katika hatari mara nne zaidi ya kuambukizwa VVU kuliko wavulana¹⁵⁰.

Kiwango kikubwa zaidi cha Magonjwa ya Zinaa yaani sexually transmitted infections (STI) yalitambuliwa kuwa (vidonda vya uzazi, Kisinono, tutuko ya genitalia, na kaswende) yanapatikana katika watu wa asili ya Weusi, na mengi za kesi hizo zilihusisha wanaoishi katika maeneo za umaskini mkubwa, hasa mijini¹⁵¹. Utafiti¹⁵² juu ya diaspora ya Wafrika inaangazia kuzuizi katika ufahamu wa matukio ya magonjwa ya Zinaa katika idadi ya watu Weusi ni kwamba data inaripotiwa na Public Health England kwa jumla ya kundi ya 'Weusi', wakati inajulikana kuwa viwango vinatofautiana katika vikundi tofauti vya Weusi.

2.6.3 Kifua Kikuu

Kifua Kikuu au Tuberculosis (TB) ni ugonjwa wa bakteria inayosababishwa na *Mycobacterium tuberculosis* (*M.tb*), ambayo mara nyingi huathiri mapafu¹⁵³. TB inaweza athiri sehemu yoyote wa mwili lakini hatari ya maambukizi hutokea tu wakati ugonjwa huo upo katika umbo/ hali hai ndani ya mapafu. Wahamiaji na makabila madogo katika Uingereza wana viwango vya juu vya TB ikilinganishwa na idadi ya watu kwa jumla¹⁵⁴.

